WFP World Food Programme


UNCDF Unlocking Public and Private Finance for the Poor

# Mafunzo ya Kifedha

Kozi fupi ya wiki 5

## Kiswahili

# Kitabu cha mwalimu




01 Chati ya mafunzo

02 Mfumo wa masomo

03 Kazi za kipato & matumizi

04 Kadi za mifano

# Jinsi ya kutumia kitabu hiki?



Chati za mafunzo



Kazi za vikundi



Kitabu cha




Kazi za



Kadi za mifano



Kuigiza



Mijadala




Kadi za mapato
& kadi za gharama




Shughuli




Mwisho wa kitengo

Utangulizi wa stadi na maarifa ya kifedha

# Kozi ya msingi





Vikao 10



Vitengo 4

**Kitengo 01:** Utangulizi
Kipindi 01
**Stadi na maarifa ya kifedha ni nini?**.................................. 03

**Kitengo 02:** Akiba
Kipindi 01
**Akiba ni nini?**.................................................................. 05
Kipindi 02
**Malengo & akiba** ............................................................ 07
Kipindi 03
**Njia tofauti za kuweka akiba**............................................... 09

**Kitengo 03:** Uendeshaji wa mambo ya kifedha ya kibinafsi
Kipindi 01
**Kuweka malengo ya kifedha**.................................................. 13
Kipindi 02
**Kupanga bajeti** .............................................................. 15
Kipindi 03
**Kufanya maamuzi kuhusu matumizi ya pesa**......................... 18
Kipindi 04
**Kufuatilia pesa taslimu kila siku**.......................................... 20

**Kitengo 04:** Huduma za kifedha
Kipindi 01
**Huduma za kifedha**............................................................ 23
Kipindi 02
**Mobile money ni nini?**......................................................... 25

## Ujuzi wa kifedha ni nini?
## Kipindi 1

Ujuzi wa kifedha ni mkusanyiko wa mbinu na maarifa vinavyomwezesha mtu kufanya uamuzi mwafaka kuhusu namna ya kutumia pesa.

Ujuzi wa kifedha huzingatia ujuzi, maarifa, mbinu, na tabia za kifedha vinavyohitajika ili kufanyia uamuzi mwafaka wa kifedha ili kufikia kilele cha usitawi wa kifedha kwa mtu binfsi.

Kuwa Kuwa mtu mwenye ujuzi wa kifedha ni pale ambapo unafahamu kanuni za msingi za kifedha kama vile:

- Kuhifadhi pesa zako
- Wapi na namna ya lufungua akaunti
- Kuweka kumbukumbu mwafaka za shughuli zako za kifedha
- Namna ya kupata usaidizi wa kifedha

**Kwa nini ni muhimu kuwa na ujuzi wa kifedha?**

- Mtu mwenye ujuzi wa kifedha huwa anafanya uamuzi mzuri katika shughuli zake za kifedha

- Ana pesa za kugharimia dharura na mambo muhimu (kutoka hifadhi yake)

- Pia utaweza kukopa pesa kwa urahisi bila vikwazo


- Kuna unwezekano mkubwa kwamba mtu huyu hatafanya uamuzi mbaya wa kifedha utakaodhuru familia yake na biashara yake

- Kuwa na maarifa yanayoongeza namna mtu huyu anavyofahamu shughuli zake za kifedha

- Kuwa na mbinu zinazomwezesha kutekeleza maarifa yake ya ujuzi wa kifedha ili kutawala pesa zake

- Kupata ukakamavu na tabia chanya inayomwezesha mtu kuwa na uhakika kuwa atafanya uamuzi mzuri wakati akishughulikia pesa zake










**Ujuzi wa kifedha unamwezesha mtu:**

- Kufahamu mipango muhimu ya kifedha utakayohitaji maishani mwako

- Kufahamu istilahi muhimu za kifedha kama riba jumlishi, faida ya uwekezaji, hatari, na kusambaza uwekezaji, na nyinginezo

- Kujadili pesa na mambo ya kifedha—hata kama kawaida hupendi kujadili mambo haya

- Kufanya machaguo bora kuhusu kuhifadhi pesa, kutumia pesa, na kutawala madeni

- Kuitikia vyema mabadiliko yanayoathiri afya yako ya kifedha ya kila siku



Chati 01
**Ni mambo gani yanayozingatiwa katika Ujuzi wa kifedha?**

**Sema:**
Ujuzi wa kifedha huanzia kwa kutupatia maarifa kuhusu namna ya kutawala vyema fedha zetu na yote tunayoyahitaji ili kufanyia uamuzi bora wa kifedha. Lakini lazima tutekeleze maarifa hayo katika maisha ya kila siku, na kuyatumia kufanya uamuzi mzuri.

Kwa hiyo, ujuzi wa kifedha unatutaka tugeuze mienendo yetu ya kifedha tuliyonayo sasa na kuanza kutumia mienendo mipya. Mabadiliko haya hutokea hatua kwa hatua na ni lazima tuwe na hamu ya kubadilisha mienendo fulani, ili kuepukana na matatizo yetu ya kifedha na kutimiza malengo yetu ya kifedha.

Mienendo ya sasa

- Kutokuwa na hifadhi ya kesho
- Kuhifadhi hakulingani na malengo ya
- hifadhi hiyo
- Kupata mikopo ya kugharimia mipango
- ya haraka
- Kushindwa kuchagua biahsara mwafaka ya kuwekeza

Mienendo inayofaa

- Kuwa na mpango wa matumizi, bajeti na kuitumia kutawala fedha
- Kuwa na mpango wa kuhifadhi wenye malengo mwafaka
- Kuwa na mfuko wa kugharimia mipango ya haraka
- Chooses the right investment



**Mwisho wa somo la 01**

## Hifadhi ni nini?
## Kipindi 1

Uliza vikundi maana ya hifadhi. Wahimize kusema majibu yao kwa sauti. Zingatia majibu yafuatayo kupanua yale waliyosema:

- Pesa zinazowekwa kando sasa ili kutumika siku za mbele
- Kuwekeza kwenye wanyama au ardhi ambavyo vitauzwa pesa zikihitajika
- Ni njia ya kujenga rasilimali
- Ni sehemu muhimu ya kutawala pesa

Uliza:
Ni sababu gani kuu zinazofanya watu kuhifahi pesa? Wahusika waseme majibu yao kwa sauti. Zingatia majibu yafuatayo kupanua yale waliyotaja:

- Ugonjwa
- Harusi
- Mazishi
- Uzee
- Mahitaji ya haraka
- Nyumba Masomo
- Kuborehsa nyumba
- Kuwekeza biashara Kuzaa
- Kwenda likizo

**Uliza:**
Unajua maana ya kuhifadhi pesa? Wahusika waseme majibu yao kwa sauti.

**Sema:**
Kuhifadhi ki kuweka pesa kando ili kuzitumia siku za mbele. Unaweza kuhifadhi pesa au mali.



Kazi ya vikundi
**wambie wanafunzi kujipanga kwa vikundi 2 au 3**

Wape wanafunzi dakika kama 5-10 kufanya zoezi hili. Kila kikundi kinaandika orodha ya njia bora za kutumia na kuhifadhi pesa.

Uliza vikundi kusema majibu yao kwa sauti. Tumia majibu yafuatayo kupanua mapendekezo waliyotoa:

- Fanya bajeti ya wiki au mwezi ujao. Hii inamanisha unaorodhesha pesa unazotarajia kupata na unazotumia, na kwamba unapanga njia za matumizi ya pesa hizo. Onyesha ni pesa ngapi utakazohifadhi kila siku, wki au mwezi

- Fuata mpango huu wa kuhifadhi pesa

- Kabla hujatumia pesa, jiulize kama kweli unahitaji hichokitu unachotaka kununua.

- Usinunue kitu kama kweli hukihitaji

- Usipotumia pesa ambazo si lazimia kuzitumia, ziweke kando kwa matumizi ya siku za mbele. Usizitumie kwa sababu unaweza kuzitumia!

- Pia ni bora kuhifadhi pesa ndogo sana kuliko kutohifadhi chochote

- Andika kila pesa ulizohifadhi na kutumia kila siku, wiki au mwezi

- Chunguza matumizi yako ya kila siku na kuamua njia za kuyapunguza ili kuweza kuhifadhi pesa zaidi

- Weka hifadhi yako benkini au kwenye shirika la wahifadhi. Hii itakusaidia kutotumia pesa hizo, na itakuwia rahisi kuhifadhi pesa

## Bainisha malengo ya kuhifadhi

Malengo ya familia yako ya kuhifahi pesa ni yapi? Uliza kikundi kusema majibu yao kwa sauti. Baada ya wanafunzi kusema malengo yao, eleza yafuatayo:

- Malengo ya kuhifadhi pesa yanaweza kuzingatia muda mfupi au mrefu
- Malengo ya muda mfupi ni yale yatakayotimizwa ndani ya mwaka 1, kwa mfano, kulipa karo ya shule
- Malengo ya muda mrefu ni yale yatakayochukua zaidi ya mwaka 1 kutimiza, kwa mfao, kurekebisha nyumba au kununua nyumba.




Chati 02
**Kubainisha malengo**

**Kutayarisha mpango wa kuhifadhi pesa wa familia yako**

**Sema:**
Fikiria malengo ya familia yako ya kuhifadhi pesa. Ni mpango gani unaotaka kuhifadhia pesa kwa muda mfupi? Mna malengo gani ya kutimiza kwa muda mrefu? Ili kutimiza malengo yako ya kifedha, utahitaji mpango ambao unabainisha kila shabaha, kiasi cha pesa zinazohitajika kutimiza shabaha hiyo, na kiasi cha pesa utakazohifadhi kila wiki au mwezi kumaliza kipindi fulani.

Ili kufanya mpango huu, lazima ukague kipato chako, fahamu kiasi ambacho unaweza kuweka kando kama hifadhi, na uamue sababu za kuhifadhi pesa. Ni malengo yapi ambayo ni muhimu zaidi kwako? Mpango bora utakusaidia kujua la kufanya, na kuimarisha nia yako ya kuhifadhi na kufaulu katika kutimiza malengo yako ya kuhifadhi pesa.



Kitabu cha mazoezi: urakasa 02
**Ndoto zangu**

Wambie wanafunzi kutafuta ukurasa husika katika kitabu cha mazoezi. Chagua mtu mmoja kutoka kikundi na kumwuliza lengo lake la kuhifadhi pesa la muda mfupi na moja la muda mrefu. Chora na kuandika malengo hayo katika kitabu kwa mwandiko wazi.

- Wape wanafunzi mfano wa lengo la muda mfupi na la muda mrefu. Muda wake na kiasi unachoweza kuhifadhi vitaamua kama ni lengo la muda mfupi au la muda mrefu
- Taja kwamba lazima kila mwanafunzi abainishe lengo la kuhifadhi pesa la kutimiza kwa muda mfupi mwishoni mwa kozi ya wiki tano ambalo litafuatiliwa wakati wa kipindi cha kupima na kutathmini



Kitabu cha mazoezi: urakasa 03
**Malengo & Hifadhi**

Tafadhali kumbuka kwamba mkebe ni mfano mmoja tu wa mahali pa kuhifadhi pesa, taja kwamba kuna njia zingine na zilizobora zaidi za kuweka pesa kuliko kuziweka nyumbani. Chagua mtu

kutoka kikundi na kumwuliza baadhi ya malengo yake ya muda mfupi. Andika malengo haya kwenye safu ya kwanza kwa mwandiko bora. Kwa kushirikiana na kikundi, jaza viasi mwafaka vya pesa kwenye sehemu zingine za ukurasa na waonyeshe namna ya kutumia kifaa hiki.

**Eleza:**
Vifaa hivi vitakusaidia kupanga vyema na kukagua kama malengo unayofikiria yanaweza kutimilika au la. Endelea kufikiria ni kiasi gani cha pesa unazotakiwa kuhifadhi ili kutimiza malengo yako kwa kipindi ulichoamua.




Kazi ya nyumbani:
**Kila mwanafunzi anatakiwa kunakili vielelezo viwili kwenye vitabu vyao, kuvijaza na kuja navyo katika somo linalofuata.**

Mwalimu afuatilie mara kwa mara na kuchunguza ikiwa wanafunzi wameweza kuhifadhi, na wanajitahidi kuimarisha malengo yao ya muda mfupi ambayo yataboreshwa mwishoni mwa kozi hii.

## Kipindi 2

Waombe wanafunzi kukuonyesha zoezi walilofanyia nyumbani. Hakikisha kwamba kila mtu amepata majibu sahihi na uangaze pale wasipofahamu kama wapo. Kwa kielelezo cha Malengo na Hifadhi katika ukurasa wa 2 kwenye kitabu cha mazoezi, hakikisha kwamba viasi vilijazwa vyema. Kama kuna yeyote kwenye kikundi ambaye hakujaza kielelezo vizuri, mwambie aje baada ya somo ili umwelezee tena au rudia kazi hiyo kwa kukundi kizima kabla ya kuendelea. Unaweza kutumia mwanafunzi aliyeelewa vyema kuwaelezea wale ambao hawajaelewa.

**Eleza:**
Uliza kila mwanafunzi kama jumla ya pesa anazotakiwa kuhifadhi kila mwezi zitatosha kutimizia malengo yao? Pia ikiwa waliweza kuhifadhi kiasi hicho cha pesa mwezi uliopita? Kwa wanafunzi wasioweza kuhifadhi kiasi hicho, washauri kujaza jedwali lile tena na kugeuza malengo ya kuhifadhi pesa kwa kila mwezi.

Kila mwanafunzi anafaa kufahamu kwamba kawaida watu wanaweka malengo makubwa yasiyoweza kutimizwa, na kwamba ni muhimu sana kuweka malengo yanayoweza kutimizwa na ambayo hayakiuki mipaka.

**Kuorodhesha malengo ya kuhifadhi pesa kulingana na umuhimu wake**

**Eleza:**
Kagua tena malengo ya kuhifadhi pesa uliyoweka, kwani, huwa ni vigumu kuyatimiza yote. Kwa hiyo, ni muhimu kupanga malengo yako kwa kuzingatia yapi ni ya muhimu zaidi kuliko mengine. Tumia namba 1 kwa lenhgo muhimu zaidi, na namba 2 kwa lengo muhimu linalolifuata, endelea hivyo mpaka mwisho.

Vikundi vikisha maliza, waombe wanafunzi 2 au 3 kujibu yafuatayo:

**Kwa nini umeyapanga melengo ya kuhifahi pesa namna ulivyoyapanga?**

Jadili umuhimu wa kuhifadhi pesa kwa ajili ya mahitaji ya msingi kama matibabu, elimu na nyuma.

**Kwa nini ni muhimu kuweka malengo ya kifedha yasiyokiuka mipaka?**

Hakikisha majibu yafuatayo yametajwa:

- Itakusaidia kuambua ni mambo gani muhimu utakayokutumia pesa zako kwa siku za mbele
- Itakupa mwelekeo wa kutumia na kuhifadhi pesa
- Itakusaidia kujiepusha na kuishiwa na pesa kwa ghafla.
- Itakusaidia kujiepusha na hali ya kubanwa kifedha
- Itakusaidia wewe na familia yako kuwa na malengo sawa ya kifedha itakusaidi



Mfano 01
**Hofadhi ya Omar**

**Kuhifadhi pesa za kugharimia dharura**

Ni dharura gani ambazo unafikiri zitakuwa na athari mbaya zaidi? Taja dharura mbalimbali ambazo wanafunzi wametaja kwa sauti.

Ni dharura gani ambazo huenda ukapata ndani ya mwaka mmoja? Dharura hizo zitakuwa na athari gani kwa familia zikitokea?



Kazi ya vikundi:
**Gawa wanafunzi katika vikundi vidogovidogo vya watu 2 au 3. Vipe vikundi dakika 5-10 kujadili maswahi haya.**

Wakati wanafunzi wakijadiliana, chora jedwali lenye safu mbili zenye vichwa 'aina ya dharura' na 'athari zake'. Uliza kila kikundi kuripoti kuhusu aina tofauti ya dharura na athari zake. Andika mawazo yao kwenye karatasi.

**Sema:**
Dharura inamanisha kwamba kuna matunizi ya haraka ambayo yataathiri familia. Matumizi haya yanaweza kuwa pamoja na matibabu, kujenga tena baada ya maafa, kununua vitu vipya baada ya kuibiwa au kulipa mkopo baada ya kupoteza biashara. Kama mkuu wa familia hawezi kufanya kazi kwa sababu ya dharura hiyo, familia itazidi kupoteza pesa.

**Uliza:**
Ni vikwazo gani ambavyo familia itakuta wakati ikijaribu kuweka kando kiasi hiki cha pesa?

Unawapa ushauri gani?

Andika vikwazo hivyo na ushauri huo kwenye karatasi.

**Sisitiza hoja hii:**
Kumbuka, madhumuni ya mfuko wa dharura ni kugharimia dharura ndogondogo. Wengi wetu hatutaweza kuhifadhi pesa za kutosha ili kugharimia dharura kubwa sana kama kupoteza nyumba au mashamba.

**Njia mbalimbali za kuhifadhi pesa**



Chati 03
**Mahali pa kuhifadhi ?**

Wape fursa baadhi ya wanafunzi kutoa majibu yao kabla hujatoa majibu yafuatayo:

- Kwenye akaunti katika benki kubwa au shirika dogo la kuhifadhi na kukopesha pesa au benki ndogo. Hili ni shirika rasmi lililoidhinishwa kuhifadhi pesa. Ni njia salama ya kuweka pesa zako. Zinatoza ada ya kila mwezi au kila mwaka

- Shirika la kuhifadhi na kukopesha pesa au kikundi chochote kingine cha hifadhi

- Watu kutoka kijiji kimoja au kikundi cha wakulima wanaweka pesa zao pamoja ili kupata riba. Mashirika ya kuweka na kukopesha pesa yanakopesha wanachama pesa hizo na kupata riba. Kila mwanachama atapata mgao wake kutoka riba hiyo

- Kuhifadhi pesa kwenye Shirika la kifedha la SACCO. SACCO ni shirika la kuhifadhi na kukopesha pesa. Huwa limesajilishwa kisheria na lina kamati na ofisi na mfumo rasmi wa utawala. Shughuli zake ni za kirasmi na zinaendeshwa kwa kufuata sera na kanuni rasmi. Linakuwa na akaunti kwenye benki kubwa

- Kuweka pesa nyumbani, kwenye kisanduku au mkebe, chini ya godoro, au kwenye shimo ndani ya ardhi nyumbani. Njia hii ni njia isiyo salama kabisa kuliko njia zingine

- Rasilimali kama mifugo na ardhi ni njia ya kuhifadhi pesa kwa sababu vinatunza thamani na vinaweza kuuzwa tena (kwa bei ile ile au zaidi) katika siku za mbele.



Uliza jirani yako:
**Una dakika moja kumwuliza jirani yako ni njia gani ambayo anafikiri ndiyo bora zaidi ya kuhifadhi pesa, na kwa nini?**

Mpe kila mwanafunzi dakika 1-3 kujadiliana na jirani yake, kisha waulize wanafunzi wachache kusema majibu ya majirani yao.

## Kipindi 3

**Uliza:**
Unakumbuka njia mbalimbali za kuhifadhi pesa tulizojadili katika kipndi cha awali? Wape fursa baadhi ya wanafunzi kutoa majibu yao.



Chati 03
**Mahali pakuhifadhi?**

## Uzuri na ubaya wa njia mbalimbali za kuhifadhi pesa

**Sema:**
Sasa tutajadili uzuri na ubaya wa njia mbalimbali za kuhifadhi pesa. Tafadhali jaribu kuzifahamu vizuri na uliza kama kuna kitu usichoelewa.

**Uliza:**
Kuhifadhi pesa benkini kuna uzuri na ubaya gani?

**Uzuri:**
- Benki ni mahali salama pa kuweka

- Benki zinaweka vizuri kumbukumbu zako za kuweka na kutoa pesa

- Unaweza kupata mkopo kutoka benki kama umeweka pesa huko kwa muda fulani

**Ubaya:**
- Unapewa riba ndogo sana kwenye pesa zako, kwa hiyo, haisaidii pesa zako kuongezeka kwa haraka

- Unaweza kupita hatua ndefu ili kufungua akaunti

- Huwa unalipa ada kila mwezi/mwaka ukiwa na akaunti benkini

- Kama mtandao umekatika benkini hutaruhusiwa kutoa pesa zako

- Unaweza kutaka kutoa pesa kutoka benki au ATM lakini viko mbali sana kutoka nyumbani

**Uliza:**
Kuhifadhi pesa kwenye shirika la kuhifadhi na kukopesha kuna uzuri na ubaya gani?

**Uzuri:**
- Ni rahisi sana kupata mkopo

- Ni rahisi sana kuhifadhi kwani wenzako wanakupa moyo pamoja na kuhifadhi pamoja

- Unapata riba bora kwenye hifadhi yako

- Ni salama kuliko kuhifadhi chini ya godoro au kwenye kisanduku nyumbani

- Ukiwa na dharura unaweza kupata pesa haraka bila kutozwa riba

- Shughuli za kifedha zinafanywa kwa haraka na kwa uwazi

- Unapewa ushauri na usaidizi ukipata shida

**Ubaya:**
- Kuna hatari ya wizi kutendeka kama wanachama hawajuani vizuri au wanachama wasipofuata masharti na kutofuatilia shughuli za shirika

- Unatakiwa kuhudhuria mikutano mara kwa mara na kwa hiyo watu wasio na muda huo watashindwa kuwa wanachama

- Masharti ya shirika kawaida huwabana watu wenye nia ya kujiunga kama tayari idadi ya wanachama imefika 30

- Pesa unazohifadhi unaweza kuzipata kwa urahisi, kwa hiyo unaweza kuitikia hamu ya kuzitoa na kuzitumia

**Uliza:**
Kuhifadhi pesa kwenye shirika la SACCO kuna uzuri na ubaya gani?

**Uzuri:**
- Una nafasi za kupata huduma bora kama mikopo mikubwa

- Ni mahali salama pa kuweka pesa

- Hatua za kupata mkopo ni fupi na rahisi

- Hakuna ada ya akaunti ya kila mwezi, na pale ambapo ipo, huwa ni ndogo sana

- Mashirika ya SACCO hayana mikutano ya mara kwa mara isipokuwa mkutano mkuu wa mwaka

**Ubaya:**
- Ili kuwa mwanachama, unatakiwa kununua hisa na kulipa ada fulani
- SACCO hazipatikani kila mahali

**Uliza:**
Kuweka pesa kisandukuni au chini ya godoro nyumbani kuna uzuri na ubaya gani?

**Uzuri:**
- Hakuna ada ya kila mwezi
- Unaweza kupata pesa zako kwa haraka kama una dharura

**Ubaya:**
- Kuna hatari kubwa ya pesa

- Hutapata riba yoyote kwenye pesa unazohifadhi

- Huwezi kupata pesa zaidi kuliko zile ulizoweka kisandukuni

- Pesa zako ziko karibu sana nawe na ni rahisi sana kuitikia hamu ya kuzitumia

**Uliza:**
Kuhifadhi kwa kununua mifugo au ardhi kuna uzuri na ubaya gani?

**Uzuri:**
- Hakuna ada za kila mwezi au hatua ngumu

- Unaweza kuuza mifugo au ardhi ukipata dharura

- Mifugo na ardhi vinawza kuongeka kwa thamani na kukupa nyongeza ya pesa, kwa mfano kukodisha ardhi kwa watumiaji

**Ubaya:**
- Kuna hatari ya magonjwa au vifo kwa mifugo, au hata wizi

- Unahitaji pesa kutunza mifugo na pengine ardhi



Mchezo
**Kwa nini ni muhimu kuhifadhi?**

Wambie wanafunzi kujigawa kwenye vikundi 3 au 4 kulingana na ukubwa wa darasa.

**Sema:**
Tutaigiza machezo ambapo mhusika mkuu atatumia pesa zaidi ya kiasi anachotatarajiwa kutumia.

Toa kila mojawapo ya mada zifuatazo kwa kikundi fulani. Pia unaweza kubuni mada.

**Mada 1:**
Karo ya shule imepandishwa na lazima ilipwe kabla ya watoto kwenda shuleni. Wahusika: mke, mwalimu, mume, watoto

**Mada 2:**
Mke anaugua na kuhitaji matibabu. Wahusika: mume, mke, watoto, daktari

**Mada 3:**
Watoto wamekuja likizoni na wanahitaji chakula bora. Wahusika: mke, mume, watoto.

**Mada 4:**
Mwuzaji anataka pesa ndipo alete vitu vinavyohitajika nyumbani. Wahusika: mume, mke, watoto, mwuzaji.

Julisha vikundi 1 na 2 kwamba mhusika mkuu amehifadhi pesa. Julisha vikundi 3 na 4 kwamba mhusika mkuu hajahifadhi pesa zozote.

Vikundi vichukue muda wa dakika 10 kutayarisha na kujaribu mchezo wao.

Uliza kila kikundi kuigiza mchezo wao mbele ya darasa zima.

Baada ya vikundi vyote kuigiza, uliza darasa zima maswali yafuatayo:

- Kuhifadhi pesa kuna uzuri gani?
- Je, huwa ni rahisi kupata pesa za
- kugharimia dharura ukiwa hujahifadhi pesa?
- Utapata matatizo gani usipopata pesa unapokuwa na dharura?
- Mtu akikukopesa pesa kwa dharura, atakuomba umpe nini?
- Je, ni bora kukopa pesa kwa dharura au kuwa na hifadhi?

**Ujumbe mihimu:**
Zingatia uzuri na ubaya wa kila njia ya kuhifadhi pesa kabla hujachagua njia moja inayofaa zaidi kwako.

**Kukutana na maafisa kutokamashirika ya kuhifadhi pesa**

**Sema:**
Kisha, tutajadili maswahili unayofaa kuwauliza maafisa katika mashirika ya kuhifadhi pesa kabla hujaamua ni wapi utahifadhi pesa zako. Ni muhimu sana kukutana na maafisa wa mashirika mbalimbali na kuyalinganisha kabla ya kuamua ni wapi utapachagua.



Kitabu cha mazoezi: urakasa 04
**Maswali ya kuuliza benkini**

**Muhtasari wa somo:**

Kanuni muhimu za kuhifadhi pesa:

- Hifadhi mara tu ukipata pesa. Yaani, weka pesa za kuhifadhi kando kabla hujanunua/kulipia chchote

- Jitahidi kuhifadhi 10%-20% ya kipato chako (yaani kwa kila UGX 100,000 hifadhi kiasi kisichopungua UGX 10,000-20,000)

- Usitembee na pesa nyingi mfukoni ili kujiepusha kuitikia hamu ya kuzitumia

- Usitumie pesa ovyo

- Weka hifadhi yako mahali salama ambapo huwezi kuzipata kwa urahisi sana

- Lazima ujichunge sana ndipo uweze kufaulu kuhifadhi

- Utajifunza kujichunga kupitia kujaribu na kutekeleza!



**Mwisho wa somo la 02**

## Kubainisha malengo ya kifedha
## Kipindi 1

**Sema:**
Kozi hii itakufunza namna ya kutayarisha na kutawala pesa zako. Utajifunza jinsi ya kubainisha malengo yako ya kifedha, kutayarisha bajeti na jinsi ya kufuatilia mtiririko wa pesa zako ili kuweza kufanya uamuzi bora wa kifedha.

Watu popote walipo wanafanya kazi ili kupata pesa za kutosha za kukimu matumizi yao ya kila siku, kulipa madeni yao, kuendeleza biashara, kugharimia mahitaji ya siku za mbele kama nyumba, karo ya shule na ndoa kwa watoto wao, na kuhakikisha kwamba wana pesa za kutumia uzeeni. Kawaida huwa hakuna pesa za kutosha za kutimizia malengo haya yote.



Mfano 02
**Hali ya kifedha ya Michael na Faith**



Mfano 03
**Carol na Robert: Kutimiza malengo yao**

**Mpango wa kifedha ni nini?**
Mpango wa kifedha ni kifaa kinachokusaidia kuamua jinsi ya kuongeza kipato chako na jinsi ya kutumia pesa zako kutimiza malengo yako.

**Uliza:**
Kufanya mipango ya kifedha kunakusaidiaje na familia yako?
Toa muhtasari wa mawazo yao na hakikisha unazingatia yafuatayo:

- Inakusaidia kuamua ni wapi unataka kutumia pesa zako siku za mbele
- Inakupa mwelekeo wa kutumia na kuhifadhi pesa
- Inakusaidia kujiepusha na kuishiwa pesa kwa ghafla
- Inakusaidia kutoelemewa shughuli za kifedha

**Unaweza kufanya nini ili kutayarisha mpango wako wa kifedha?**

Waombe baadhi ya wanafunzi kutoa mawazo yao. Amua malengo au shabaha za siku za mbele, amua ni kiasi gani cha pesa wanazopata na jinsi watakavyotumia pesa kuhifadhi na kuweka ili kutimiza malengo yao.

**Chagua mifano ya matumizi ya pesa**




**Kadi za gharama**

**Uliza:**
Watu hutumia pesa zao kupitia njia gani?

Shika kazi zote za matumizi mkononi na ziweke mbele ya darasa huku wanafunzi wakizisoma moja baada ya nyingine. Wanafunzi wakimaliza kuzisoma, waombe baadhi yao kuja pale mahali kadi zilipo na kuziainisha kwa kuzipanga kwenye kategoria zinazolingana na yale matumizi ya pesa.

Kadi za matumizi ni mifano tu. Wanafunzi wanaweza kupendekeza matumizi tofauti, wakifanya hivyo, chukua kadi

moja iliyo tupu na kuandika matumizi hayo na kuiweka pamoja na kadi zingine. Chagua wanafunzi wawili kuchambua kadi za matumizi na kuziweka kwenye vikundi vinavyofanana. Wambie kwamba kadi zinazofanana waziweke sambamba zikifuatana.

Wasaidie wale wanaozipanga na kuwahimiza wanafunzi wengine kuwa wakitaja mawazo yao. Himiza wanafunzi kutoa sababu za mapendekezo yao. Baada ya kadi zote kupangwa, zipitie pamoja na darasa zima.

**Sema:**
Tazama matumizi tena. Ni matumizi gani unayolipa kwa nadra tofauti na yale unayolipa kila siku au kila wiki? Unajitayarishaje kugharimia matumizi yanayotokea kwa nadra?

Toa muhtasari wa mapendekezo yao kwa kusema:

Hatua mojawapo kati ya hatua bora za kutawala pesa ni kujitayarishia matumizi yasiyotokea mara kwa mara. Mumetaja njia nyingi ambazo hili laweza kufanyika, mkiwemo kuhifadhi pesa na kutonunua vitu fulani hadi unapopata pesa za kuvigharimia.

**Tambua mifano ya vyanzo vya pesa**

**Sema:**
Tumezungumzia namna mbalimbali za kutumia pesa. Sasa tutajadili wapi pesa hizo hutoka.



Kadi za mapato

**Pesa zinatoka wapi?**

Shika kadi za vyanzo vya pesa mikononi mwako na kuziweka mbela ya darada moja baada ya nyingine huku wanafunzi wakizitaja. Aina za vyanzo vya pesa ni mifano tu. Wanafunzi wanaweza kupendekeza vyanzo tofauti vya pesa, wakifanya hivyo, chukua kadi moja iliyo tupu na kuandika vyanzo hivyo na kuiweka pamoja na kadi zingine. Chagua wanafunzi wawili kuchambua kadi za vyanzo vya pesa na kuziweka kwenye vikundi vinavyofanana.

**Uliza:**
Ni vyanzo vya pesa vipi ambavyo si vya mara kwa mara? Kwa nini?

Waombe wanafunzi kujitolea kuzungumzia vyanzo vyao vya pesa visivyo vya mara kwa mara. Chagua kadi zenye vyanzo walivyotaja.

Unapopata kiasi kikubwa cha pesa kwa nadra, unapanga kuzitumiaje kugharimia matumizi kwa mwaka mzima?

Toa muhtasari wa majibu ya wanafunzi kisha julisha darasa zima:

Ni jambo zuri kupata kiasi kikubwa cha pesa mara moja. Ni muhimu sana kulipa madeni, kuhakikisha unaweza kugharimia mahitaji ya msingi na kuhifadhi pesa ili kugharimia matumizi ya siku za mbele

**Eleza:**
Katika vipindi vinavyofuata tutajifunza maana ya bajeti na namna ya kuitayarisha. Kifaa hiki kitakusaidia kujitayarishia kipato na matumizi vya kila siku na vya nadra.

**Bajeti ni nini?**

Bajeti ni muhtasari wa pesa zinazotarajiwa na namna zitakavyotumiwa kwa kipindi fulani.



Chati 04
**Kutayarisha bajeti ya**

**Sema:**
Tuko hapa kujifunza namna ya kutumia pesa vizuri. Bajeti ni kifaa muhimu cha kutimizia lengo hilo. Ni mpango unaogawa pesa zako katika matumizi mbalimbali ya muhimu, pesa za kuhifadhi na za kuwekeza katika kipindi fulani.

Ili kuandaa bajeti vizuri, lazima tujue kiasi cha pesa zinazoingia na jinsi tunavyotaka kuzitumia katika muda fulani tutakaochagua. Ili kutunga bajeti, ni muhimu kutambua na kupanga matumizi.



Kitabu cha mazoezi: urakasa 07
**Kulinganisha Kipato na matumizi**




Kazi ya nyumbani:
**Kila mwanafunzi afanye zoezi la kulinganisha kipato na matumizi na famila yake nyumbani**

Wajulishe wanafunzi wakija kwenye kipindi kinachofuata, waje na vitabu vyao vikiwa na jedwali lililojazwa vizuri.

## Kipindi 2

Anzisha kipindi kwa kuuliza wanafunzi wote kuonyesha zoezi la kulinganisha kipato na matumizi walilofanya na familia yao nyumbani.

**Bajeti ina umuhimu?**

Bajeti:
- Inakuwezesha kugawa pesa zako kwa aina mbalimbali za matunizi
- Inakusaidia kufanya uamuzi kuhusu kutumia na kuhifadhi pesa
- Inakusaidia kutumia pesa zako kwa uangalifu na kwa utaratibu
- Inakuwezesha kudhibiti shughuli zako zakifedha
- Inakusaidia kupanga na kutawala pesa zako kwa njia bora zaidi
- Inakusaidia kuweka mipango imara ya siku za mbele na kutimiza malengo yako ya kifedha

**Uliza:**
Hivi sasa unatumia njia gani kutawala pesa na matumizi ili kugharimia mahitaji ya familia yako?

Ni hatua gani zinazoweza kukusaidia kuboresha kutunga na kufuata bajeti katika nyumba yako?

Wanafunzi wape dakika kama 5 kujadiliana. Uliza wanafunzi 3 au 4 kujitolea kutoa mawazo yao kwa darasa zima. Toa muhtasari wa mawazo yao na uhakikishe hoja zifuatazo zimetajwa:

Njia za kutunga na kufuata bajeti:

- Andika vyanzo vyote vya pesa
- Andika matumizi yote
- Fanya mipango mapema ili kujiepusha na kutumia pesa zaidi ya kipato
- Hifadhi pesa za ziada ili kugharimia matumizi ya siku za mbele kipato kitakapopunguka

**Sema:**
Leo tumefafanua zoezi la kuandaa bajeti na katika kipindi cha awali tulizungumzia sehemu muhimu za bajeti; pesa zilizoandikwa kwa kuzingatia kipato na matumizi, pesa zilizoandikwa kwa kuzingatia aina ya matumizi kwa mfano mahitaji ya msingi, kulipa mkopo, biashara na matumizi ya hiari. Tuliona namna bajeti inavyokuwa na kipengele cha pesa za kuhifadhi. Tulizungumzia pia jinsi sote tunavyotawala pesa zetu na hatua tunazoweza kuchukua kuboresha bajeti zetu.

**Hatua za kuandaa bajeti:**

- Kagua malengo yako ya kifedha
- Kadiria kiasi cha pesa kwa kuzingatia chanzo chake
- Andika matumizi yote na kiasi cha pesa zinazohitajika kugharimia kila matumizi
- Hakikisha kwamba matumizi yako hayazidi kipato chako
- Amua kiasi cha pesa utakazohifadhi
- Review and adjust as needed



Chati 05
**Hatua za kuandaa**



Mfano wa 04
**Sandra ameandaa**

## Kuandaa bajeti



Kitabu cha mazoezi: urakasa 08
**Makadirio ya bajeti ya familia**

Unakadiria kupata pesa ngapi na kutumia pesa ngapi katika kipindi cha mwezi 1?

Chagua mwanafunzi darasani na mwulize anakili jedwali na kuliweka kwa kitabu chake na ajaze viasi vya pesa kwa kuzingatia kipato chake na matumizi yake ya sasa.

Wambie wanafunzi wengine darasani kutazama kwa makini na wanaweza kuuliza maswali wakati wowote wasipoelewa. Wakati ukieleza kila hatua, waonyeshe jinsi ya kutekeleza zoezi hili kwa kurejelea mfano wa mwanafunzi yule.

**Kipato**

Fafanua vyanzo vya kipato kwa kurejelea mfano wa makadirio ya bajeti ya familia na uhakikishe kwamba vimejazwa kwenye safu ya upande wa kushoto. Kama chanzo chochote cha pesa hakikujazwa, basi, mwanafunzi anaweza kufuta chanzo kisichofaa kwake na kujaza kile kinachofaa kwenye mstari huo. Baadhi ya vyanzo hivi vinaweza kuingiza pesa kila mwezi na vingine vinaweza kuingiza pesa mara moja au mbili katika mwaka.

Kadiria pesa zinazotarajiwa kila mwezi kutoka kila chanzo cha pesa na uzijaze kwenye kisanduku mwafaka kwenye ukurasa. Baadhi ya pesa zinaweza kuingia kama kufurushi mara chache ndani ya mwaka. Ili kujua namna hivyo vifurushi vinavyoweza kugawika kwa mwezi, hesabu jumla ya pesa unazopata kwa mwaka mzima na uzigawie 12.

Pata jumla ya pesa zote za kila mweza.

Sasa, uliza wanafunzi wote kujaza majedwali yote ya kipato. Tembea darasani ukitoa usaidizi kwa yeyote anayehitaji msaada. Wanafunzi watumie kikokotoo kwenye simu zao, kama wanahitaji kikokotoo, kuhakikisha kwamba viasi walivyojaza ni sahihi.

**Aina za matunizi**

Kwenye ukurasa wa bajeti ya familia, andika matumizi ya kila kategoria ya matumizi: hifadhi (kwani tunataka wanafunzi kuweka pesa kando na kuanza kuhifadhi), kulipa madeni, mahitaji ya msingi, matumizi ya hiari, na kadhalika.

Kadiria matumizi ya kila kategoria ya mwezi mmoja. Kuna matumizi yanayotokea mara moja katika mwaka au katika kila robo ya mwaka. Iwapo kuna matumizi ya nadra kama hayo (kwa mfano karo ya shule), ni muhimu kuyagawa kwa mwaka mzima katika bajeti.

Kufahamu namna ya kuyagawa matumizi ya nadra kwa mwezi, hesabu jumla ya matumizi ya kila mwaka na kuyagawia 12.

Weka pamoja jumla ya matumizi ya kila mwezi kwenye ukurasa wa bajeti ya famila.

Sasa, wambie wanafunzi wote kujaza majedwali yote ya matumizi. Tembea darasani ukisaidia mwanafunzi yeyote anayehitaji usaidizi.

Wanafunzi watumie kikokotoo kwenye simu ili kuhakikisha kwamba viasi vya pesa walivyojaza ni sahihi.

**Linganisha kipato na matumizi**

Toa jumla ya matumizi ya kila mwezi kutoka jumla ya pesa zinazotarajiwa kila mwezi.

**Uliza:**
Utafanya nini ikiwa kipato kinazidi matumizi? (Hifadhi pesa zaidi, lipa madeni yote)

Utafanya nini iwapo matumizi yanazidi kipato? (Punguza matumizi, tafuta njia za kupata pesa zaidi hadi utakapodhibiti matumizi yako)



Chati 06
**Kulinganisha kipato na matumizi**

**Sema:**
Hakikisha kwamba kiasi unachoweka kwenye bajeti nikile unachoweza kuhifadhi kila mwezi katika nafasi ya hifadhi. Kiasi cha kuhifadhi kwa kila mwezi kiwe kiasi kilichofikiwa kutokana na jedwali la malengo na hifadhi. Wakumbushe wanafunzi kwamba hifadhi hiyo inahitajika ili kutimiza malengo yao.

Kuandaa bajeti kunasaidia familia kuwa wanakumbuka kipato na matumizi yao ya kila mwezi wakati wote na hili litawasaidia kutimiza malengo yao.




Kazi ya nyumbani:
**Wambie wanafunzi kujaribu kujaza jedwali lile tena wakishirikiana na watu wengine kwenye familia yao.**

Wanatakiwa kujaza viasi vya pesa kwenye ukurasa huu vinavyokaribia sana na viasi vyenyewe vya pesa wanazopata au kutumia.

## Kipindi 3

Anza kipindi hiki kwa kuuliza darasa kuonyesha zoezi walilopewa kufanyia nyumbani. Kagua kuhakikisha wanafunzi wote walijaza majedwali yao vizuri. Kukiwa na haja, sahihisha makosa ya kawaida yote kabla hujaendelea.



Mfano wa 05
**Peter anafuata bajeti yake**

### Kufanya uamuzi wa matumizi

**Sema:**
Sasa tutazungumzia namna ya kuchagua matumizi ya kutanguliza. Ni watu wachache sana duniani ambao wana pesa nyingi sana kiasi kwamba wanaweza kulipia kila kitu wanachotaka kununua au kufanya. Wengi wetu tunafanya uamuzi mgumu wa kuchagua kati ya matumizi muhimu, hasa wakati ambapo kipato chetu hakiwezi kugharimia matumizi yetu yote. Hakuna majibu sanifu tunapojadili swala la uchaguzi wa matumizi ya kutanguliza, lakini kuna mwongozo wa jumla.

Leo tutajadili namna unavyofanya uamuzi huu sasa, kisha tutataja baadhi ya njia za kawaida za kukusaidia kubainisha namna ya kuamua ni matumizi yapi utakayotanguliza, na kuweza kudhibiti shughuli za koza kifedha katika siku za mbele.

Utaamuaje ni vitui gani ambavyo ni vya muhimu zaidi na ndivyo utagharimia mwezi huu?



Kazi ya vikundi:
**Wanafunzi wanaunda vikundi vya watu 2 au 3 na kujadili namna wanavyotaka kutanguliza baadhi ya matumizi haya**

- Yapi ndiyoya muhimu zaidi?
- Yapi ambayo si ya muhimu sana?

Una maswali yoyote?

Zunguka darasani ukijibu maswali ya kila kikundi. Baada ya vikundi vyote kumaliza, uliza vikundi viwili kuwasilisha uamuzi wao. Wambie wawasilishe matumizi waliyotanguliza yakifuatana kulingana na umuhimu wake na waeleze kwa nini waliyapanga hivyo.

**Linganisha matumizi waliyotanguliza na yale ambayo wataalam wa mipango ya kifedha wanayopendekeza.**

**Eleza:**
Wataalam wa mipango ya kifedha wa-

napendekeza matumizi yatangulizwe yakifuatana hivi:

1. Kwa ajili ya malengo na mahitaji ya siku za mbele
2. Lipa madeni yote
3. Gharimia matihaji ya msingi ya kila siku

**Uliza:**
Kwa nini unafikiri wataalam walipendekeza matumizi yatangulizwe kwa kufuatana hivyo?

Chagua wanafunzi kadhaa kutoa majibu. Sisitiza hoja zifuatazo iwapo wanafunzi hawakuzitaja:

- Madeni ni hasara

- Ukishindwa kulipa deni, riba inaongezeka. Ada za kuchelewa kupipa zinaweza kuongeza kiasi cha pesa uunazodaiwa na kuongeza hatari ya kutumia pesa ambazo zingegharimia mahitaji ya msingi kutumika kulipia madeni

- Ukishindwa kulipa deni vizuri unaweza kuadhibiwa kwa kunyimwa mikopo mingine siku za mbele

- Madeni yakizidi yanaweza kuhatarisha masilahi ya familia

- Mahitaji ya msingi ya kila siku lazima yagharimiwe kwa ajili ya masilahi ya familia

- Ikiwa hakuna madeni na mahitaji ya msingi ya kulipia, pesa zilizopo zinawekwa kando kutumiwa siku za mbele au kugharimia matumizi ya hiari (kwa mfano kujiburudisha)

**Heshimu bajeti yako**


**Sema:**
Wataalam wa mipango ya kifedha wanasisitiza kwamba watu wanatakiwa kuzingatia tabia ya kulipa madeni yao yote, kulipia mahitaji ya msingi na kuhifadhi angalau kiasi fulani cha pesa. Kuna mahitaji mengi yanayong'ang'ania pesa ndogo zilizopo.

Tafadhali chukua dakika chache kufikiria hali yako ya kifedha kisha jibu swali lifuatalo:

Ni mambo yapi matatu muhimu unayotanguliza kugharimia baada ya kulisha familia yako? Kwa nini?

Chagua wanafunzi 2-3 waseme mambo waliyochagua, yakifuatana kulingana na umuhimu wake.

**Sema:**
Ni rahisi kuandaa bajeti lakini si rahisi kuifuata bajeti hiyo.



Kazi ya vikundi:
**Unda vikundi vya watu 2-3 na kujadili namna ya kujibu swali lifuatalo: Kwa nini ni vigumu kufuata bajeti?**

Kazi ya vikundi ichukue dakika 5. Chagua wanafunzi wajadili kwa nini watu wanapata shida kufuata bajeti zao.


**Sema:**
Watu wengi wana tajriba hizi. Baadi yao wanafaulu kufuata bajeti, wakitawala vizuri kipato chao na matumizi yao.

## Kufuatilia pesa zako kila siku

**Sema:**
Ili kuweza kutimiza malengo ya kuhifadhi, kuna kifaa kingine chepesi cha kukusaidia. Ni kifaa cha kufuatilia pesa zako kila siku.

Gawa mara 4 kiasi cha kuhifadhi kila mwezi ulichobainisha, na utapata kiasi unachotakiwa kuhifadhi kila wiki.

Kifaa hiki kinakusaidia kufuatilia hifadhi yako, ukiwa na uwezo wa kuhifadhi kiasi cha kila wiki, pia kitakusaidia kufuatilia na kujua ni wapi unakotumia pesa zako na kiasi cha pesa unazopata. Baada ya kutumia kifaa hiki kwa wiki kadhaa, unaweza kudurusu bajeti yako kuhakikisha viasi vyenyewe sahihi.



Kitabu cha mazoezi: urakasa 09
**Kufuatilia pesa zako kila**

Onyesha namna ya kutumia kifaa hiki, na hesabu kwa kutumia noti halisi za shilingi za Uganda kwa wale wasiojua kusoma na jaza karatasi ya kufuatilia pesa kwa siku hiyo ya wiki tu.

Eleza kwamba pesa za kuhifadhi ambazo haziwekwi nyumbani zinajazwa katika karatasi hii ili kuweza kujua kiasi chenyewe cha pesa taslimu zilizopo (katika familia). Wambie wanafunzi kukusaidia kujasa Siku 2 na Siku 3.

Hakikisha kwamba wanafunzi wote wanafahamu jinsi ya kutumia kifaa hiki na jibu maswali yoyote waliyonayo kabla hawajaondoka mwishoni mwa kipindi.




Kazi ya nyumbani:
**Wambie wanafunzi watumie kifaa hiki kwa muda wote wa kozi hii**

Wakumbushe kwamba wanafaa kujaza pesa wanazofuatilia siku hiyo mwishoni wa siku hiyo ili wasije wakasahau.

Kama hawakuwa na pesa au matumizi au pesa za kuhifadhi kwa siku fulani, basi, mwanafunzi ajaze 0. Mwanafunzi asijaze kiasi cha pesa kilicho bandia.

## Kipindi 4

(bora kifundishwe siku 2 au 3 baada ya kipindi cha 3)

Anza kipindi kwa kuwaomba wanafunzi kuonyesha kazi ya nyumbani waliyotakiwa kufanya. Chunguza kama wanafunzi wote wamejaza vizuri pesa za kufuatilia kila siku kwenye majedwali katika vitabu vyao na sahihisha makosa ya kawaida kama yapo.

Wambie wanafunzi kuendelea wakitumia kifaa hiki kila siku ili kuweza kuzoea kufuatilia pesa, kisha wajulishe kwamba wanafaa kuendelea wakitumia kifaa hiki hata baada ya kumaliza kozi.



Mfano 06
**Kisa cha Mary**

**Namna ya kufuata bajeti yako?**

- Zidi kujikumbusha mpango wako wa matumizi
- Miongoni mwa matumizi kwenye bajeti weka pia matumizi dharura

- Weka hifadhi yako mahali ambapo si rahisi kuitumia

- Weka kumbukumbu ya matumizi yako

- Hakikisha kwamba matumizi yako hayazidi kiasi ulichobainisha katika bajeti

- Ukitumia kiasi kikubwa kwenye kitu fulani, mpunguza matumizi kwenye kitu kingine

- Andika njia za kupunguza matumizi uliyopanga

- Shirikisha familia yako kwenye zoezi la kuandaa na kufuata bajeti

- Wakati ukiwekeza pesa katika biashara, fikiria utakachofanya biashara hiyo isipofaulu

**Muhtasari wa somo hili:**

Kudhibiti pesa zako vizuri, unatakiwa kufahamu vyema mahitaji ya familia yako:

- Kufuatilia kipato na matumizi yako
- Kubainisha malengo ya kifedha
- Kuandaa mpango wa kifedha.
- Mpango wako wa kifedha
- Unakusaidia kuamua matumizi ya kutanguliza katika siku za mbele, na
- Hukuwezesha kufuata mpango wako wa kutumia na kuhifadhi pesa
- Hukusaidia kujiepusha na kuishiwa na pesa ghafla
- Inakusaidia kutohisi sana mfadhaiko wa kifedha

Mambo matatu ya kuzingatia ukitumia pesa:

- Gharimia mahitaji ya kila siku kama chakula, malazi, usafiri, mavazi, matibabu, kulipa madeni, na mathitaji yasiyo ya lazima kama pombe
- Hifadhi pesa kwa ajili ya mahitaji yasiyotarajiwa, kwa mfano, dharura, matibabu, kifo, kununua mali inayouzwa kwa haraka
- Kuwekeza pesa kwenye mahali zinakowekewa ribaa kwa muda mrefu

Namna ya kufuata mpango wako:

- Zidi kujikumbusha mpango wako wa kutumia pesa
- Weka pesa za kugharimia matumizi ya dharura kwenye mpango wako
- Weka pesa ulizohifadhi mahaliambapo si rahisi kuzitumia
- Fuatilia matumizi yako, hakikisha kwamba matumizi yako hayazidi kiasi ulichopanga kutumia
- Shirikisha familia yako kwenye maandalizi na kufuata bajeti

Namna ya kutumguza matumizi:

- Punguza matumizi ya vitu visivyo vya lazima (kama pombe)
- Punguza matumizi kwenye sherehe kama harusi, matanga, na aina zingine za karamu
- Fanya mipango ya kununua mahitaji ya msingi mapema wakati bei zikiwa chini na usinunue vitu vingi kwa deni
- Usitembee na pesa nyingi au weka pesa kwenye mahali salama ili kujiepusha na shauku ya kuzimutia



**Mwisho wa somo la 03**











## Huduma za kifedha
## Kipindi 1

**Huduma za kifedha ni nini?**

Tambulisha kipindi kwa kujadili aina mbalimbali za watoaji huduma za kifedha katika jumuiya yao.

**Uliza:** Taja watoa huduma za kifedha katika jumuiya yako unakokwenda kupata huduma za kifedha?

Gawa darasa kwenye vikundi vidogovidogo. Kila kikundi kitaje mifano wanayojua.

Wanafunzi wataje mifano kama Mabenki (kama benki za Equity na Centenary) , Mashirika ya mikopo (kama Benki ya Posta na Benki ya Opportunity), mashirika ya Hifadhi na Mikopo (kama PRIDE Uganda na FINCA), SACCO, Kampuni za kukopesha pesa, na kadhalika. Pekua zaidi ili kugundua kama wanafunzi wanaweka pesa nyumbani katika vyombo maalum, au chini ya godoro, na uandike mifano hiyo kwenye orodha.

**Sema:**
Kumbuka mifano ya watoa huduma za kifedha ambayo tumejadili kisha fikiria aina za huduma wanazotoa (fikiria juu ya aina zote mbalimbali za huduma unazojua au umewahi kusikia).

**Uliza:**
Baada ya kujua watoaji huduma za kifedha, ni huduma gani za kifedha ambazo watu wa jumuiya yako hupata kutoka mashirika hayo?

Wape wanafunzi fursa ya kwenda kwaa vikundi tena. Toa karatasi kwa kila kikundi kuandika kila aina ya huduma ya kifedha wanayoijua inayotolewa na hayo mashirika ya kifedha.

Baada ya vikundi kumaliza, uliza kikundi cha kwanza kuja mbele kuwasilisha kazi yao. Vikundi vvingine vinaweza kuongezea kwenye yale yaliyosemwa na kikundicha kwanza.

Utasahihisha makosa au kutoa nyongeza kwa kujadili orodha ya huduma za kifedha zinazoweza kutolewa katika jumuiya yao ambazo zinaweza kuwa pamoja na:

**Kuhifadhi pesa:**
Akaunti tofautitofauti zinatolewa na mashirika mbalimbali ya kifedha (kwa mfano akaunti ya kawaida na akaunti ya kuhifadhi kwa muda mrefu).

**Mikopo:**
Mashirika mbalimbali ya kifedha hutoa mikopo tofautitofauti yenye masharti tofauti na kwa madhumuni mbalimbali.

**Bima:**
Huduma za bima hutolewa dhidi ya matukio mahususi, kwa mfano, ajari au kifo.

**Huduma za Malipo:**
Mashitika ya kifedha huhawilisha pesa kutoka akaunti ya mteja kwenda kwa mpokeaji aliyebainishwa, kwa mfano, kutuma pesa kwa wanafamilia au kulipa bili

Toa maelezo kwa maswali yoyote wanafunzi waliyonayo kabla ya kuendelea na sehemu inayofuata.

## Huduma ya maajenti wa benki

**Uliza:**
Maajenti wa benki ni nini?

**Eleza:**
Huduma ya Maajenti wa Benki ni njia ambayo Benki hutumia kutoa huduma kwa watu wanaokuta vikwazo kupata huduma za benki.

Huduma ya maajenti wa benki, kwa kifupi, ni pale ambapo benki inatumia huduma za ajenti kutoa huduma fulani za benki kwa niaba ya benki nje ya tawi rasmi la benki au mbali na huduma ya ATM.

Mfano wa Maajenti wa benki ni kama Wajumbe wa Benki, mashirika ya SACCO, na mengine.

Wambie wanafunzi kwamba katika huduma ya Maajenti wa Benki, pesa wanatotoa zi na maajenti wenyewe. Ajenti anatumia tu mfumo wa benki hiyo kutoa huduma kwa umma na analipwa ada fulani.

**Hatua za kupata huduma ya maajenti wa benki**

Eezea wanafunzi hatua za kutumia huduma za maajenti wa benki:

- Unatakiwa kuwa na akaunti hai kwenye benki hiyo (mteja wa benki)
- Lazima uwe na Smart Card kutoka benki yako
- Lazima uwe na namba ya utambulisho (PIN) kutoka Benki hiyo au lazima benki iwe imechukua taarifa zako kwa mfano alama za vidole vyako
- Lazima uwe na stakabadhi zinazohitajika (kwa mazingira ya wakimbizi, stakabadhi ya uthibitisho na Kitambulisho)

**Uzuri na ubaya wa huduma ya maajenti wa benki**

**Uliza:**
Huduma ya Maajenti wa Benki ina uzuri na ubaya gani? Waruhusu wanafunzi kutoa majibu yao kabla hujatoa mifano kadha.

Baadhi ya uzuri wa huduma ya maajenti wa benki:

- Ni rahisi sana na inawezekana kuweka pesa kwenye akaunti yako
- Ni rahisi kupatikana na kuweza kutoa pesa kutoka akaunti yako
- Ni rahisi sana kwa mtu kuweka pesa kwenye akaunti yako
- Hakuna haja ya kusafiri mbali kwani maajenti wapo katika eneon lako
- Unaweza kutoa pesa kwenye akaunti au kununua vitu kupitia ajenti kila unapokuwa na mahitaji
- Kama Ajenti mmoja hana pesa, unakwenda kwa mwingine aliye karibu
- Pesa zinawekwa salama kwenye akaunti yako kwa kuwa hutumwa moja kwa moja kwa akaunti yako benkini

Baadhi ya ubaya wa huduma ya maajenti wa benki:

- Ajenti wa benki anaweza kutokuwa na pesa za kutosha kukuhudumia wakati unapozitaka
- Ile mashine anayotumia inaweza kukuhudumia inaweza kuharibika au mtandao unaweza kukatika
- Vitendo vya wizi vinaweza kutokea wakati ukitoa pesa; kwa mfano, maajenti kukupa pesa chache kuliko zile ulizoagiza kutoa
- Iwapo wateja ni wachache katika eneo fulani, kutakuwa na maajenti wachache na itakuwa vigumu kupata huduma hizi
- Mtu akigundua PIN yako na pia akipata kadi yako, anaweza kutoa pesa zako kutoka akaunti bila wewe kujua

**Masharti na kanuni za huduma ya maajenti wa benki**

- Daima beba vitambulisho vyako ukienda kutoa pesa (kwa mfano kitambulisho cha uthibitisho wa mkimbizi)
- Kamwe usiandike PIN yako mahali ambapo mtu mwingine ataiona
- Daima mwulize ajenti kama ana pesa za kutosha kabla hujaanza shughuli ya kutoa pesa
- Kamwe usiweke PIN yako mahali pamoja na kadi yako ya benki
- Tumia ama alama ya kidole au PIN yako kutoa pesa au kununua chakula
- Kamwe usimwambie mtu yeyote PIN yako hata kama ni ajenti au mjumbe wa benki
- Hakikisha unapewa risiti kutoka mashine ya hata kama shughuli ya kutoa pesa imekatika
- Daima weka risiti zote za shughuli za kutoa au kuweka pesa
- Kadi yako ya benki itafungwa ukiingiza PIN mbovu mara tatu kwa kikao kimoja
- Hakikisha unaandika jina na kutia saini yako kwenye kitabu cha ajenti baada ya kuweka au kutoa pesa
- Kamwe usimwachie kadi au PIN yako ajenti wa benki
- Hakikisha kwamba umepewa kiasi sahihi cha pesa kabla hutatia saini kwenye kitabu cha ajenti
- Kamwe usiache kadi yako kwa mdeni au mwuzaji ili kuweza kukopa pesa au kupata vitu vya deni
- Kadi yako ikikataa kutumika au ikipotea, ripoti kwa benki bila kukawia
- Kamwe usilipe ada yoyote kwa ajenti ukitumia pesa taslimu, ada za benki zinakatwa moja kwa moja kutoka akaunti yako wakati ukitoa pesa

## Kipindi 2

### Huduma ya Pesa za simu ni nini?

Chati 07
**Pesa za simu?**

- Huduma ya pesa za simu ni huduma ambazo zinamwezesha mtu kutuma au kupokea pesa kiumeme kupitia simu ya mkononi
- Huduma ya pesa za simu ni njia ya haraka, salama, ada zake ni chache sana na rahisi ya kutuma pesa mahali popote nchini Uganda
- Huduma za pesa za sim ni pamoja na: kutuma pesa kutoka akaunti moja kwenda nyingine, kuweka na kutoa pesa kwenye akaunti, au kulipa bili
- Ili kutumia huduma ya pesa za simu, unahitaji akaunti ya pesa za simu, ambayo utaweka pesa zako kwa njia ya pesa za hewani, na unaweza kuzitoa kama pesa taslimu wakati wowote
- Kupata akaunti ya pesa za simu, unatakiwa kujisajilisha na mtandao wa simu fulani. Kila mtu anaweza kujisajilisha. Mitandao ya simu mbalimbali inatoa huduma za pesa za simu

Uliza wanafunzi kutoa maoni yao juu ya watoa huduma za pesa za simu mbalimbali na tajriba zao za kutumia huduma ya pesa za simu.

**Unajisajilisha vipi ili kutumia huduma ya pesa za simu?**

Chati 08
**Jinsi ya kujisajilisha kwa huduma ya pesa za simu**

**Eleza:**
Masharti ya kutumia huduma ya pesa za simu:

- Tumia simu ya mkononi yenye kadi ya simu kutoka mojawapo ya mitandao ya simu inayotoa huduma hii, kwa mfano, Airtel, MTN, Africell, na kadhalika
- Uwe na kitambulisho halali
- Uwe na kadi ya simu iliyosajilishwa kutumia huduma ya pesa za simu
- Jaza fomu ya usajili

**Hatua za kujisajilisha kwa huduma ya pesa za simu:**

- Kwenda kwa ofisi za mtandao wako wa simu (kama MTA, Airtel, Africell) wambie unataka kujisajilisha kwa huduma ya pesa za simu
- Chukua nakala ya kitambulisho chako- au pasipoti, na pichaya uso wako
- Ajenti atajaza fomu ya kusajilisha mteja mpya na utatia saini yako
- Baada ya kujaza taarifa za mteja kwenye simu, ajenti lazima akuruhusu kujaza namba siri. Utahitaji namba siri hiyo kutumia na kuingia akaunti yako ya pesa za simu
- Hakuna ada ya kujisajilisha kwa huduma ya pesa za simu

**Huduma za pesa za simu**

**Uliza:**
Nani amewahi kutumia huduma ya pesa za simu? Huduma ya pesa za simu inatumiwa kufanya nini?

**Sema:**
Huduma ya pesa za simu inamwezesha mteja aliyesajilishwa kupata huduma zofuatazo:

- Kutuma na kupokea pesa kwenda na kutoka mitandao yote ya simu
- Kutoa pesa kupitia ajenti au mashine ya ATM
- Kununua muda wa simu kwenye simu yako au kwa mtu mwingine (aliye kwa mtandao huo) kwa urahisi
- Kununua data ya kutumia intaneti
- Kufanya malipo (kwa mfano bili, bidhaa na huduma, ada na kodi za URA)
- Kufanya shughuli za benki (kujua pesa kwenye akaunti yako benkini, kutuma pesa kutoka simu yako kwenda akaunti yako benkini au kutoka benki kwenda simu yako au kwenda kwa akaunti ya mtu mwingine)

**Sema:**
Unaweza kuweka pesa kwenye akaunti kwa kutumia huduma ya pesa za simu:

- Unapotaka kuhamisha pesa kwenda akaunti yako ya pesa za simu
- Unatoa pesa taslimu kwa ajenti wa pesa za simu na unapata kisawe cha kiasi hicho cha pesa kwenye simu yako
- Ni tu wateja waliosajilishwa ambao wanaweza kuweka pesa kwenye simu
- Hivi sasa hakuna ada ya kuweka pesa kwenye akaunti ya pesa za simu nchini Uganda

**Sema:**
Mteja wa huduma ya pesa za simu anawezaje kutoa pesa kutoka kwenye simu?

- Unapotoa pesa, unageuza pesa za hewani kutoka akaunti ya simu na kuwa pesa taslimu
- Unaweza kufanya shughuli hii kwenye ajenti yeyote au kituo chochote cha pesa za simu
- Kutoa pesa kutoka akaunti yako ya simu, unatakiwa kuonyesha kitambulisho chako, uwe na simu yako, na ujue PIN yako ya akaunti ya pesa za simu
- Kawaida unalipa ada fulani ili kutoa pesa kutoka akaunti ya pesa za simu, na ada hiyo inakuwa tofauti kulingana na kiasi cha pesa unazotoa

**Sema:**
Mteja wa huduma ya pesa za simu anawezaje kutuma pesa?

- Ukiwa mteja aliyesjilishwa, unaweza kutuma pesa kwa mtu yeyote, hata kama hakusajilishwa, na hata kama hana simu
- Kutuma pesa kwa mtu mwenye akaunti ya pesa za simu anayetumia mtandao kama wako, atapokea pesa kwenye kwenye akaunti ya simu yake, na atapokea ujumbe wa simu
- Kutuma pesa kwa mtu asiyesajilishwa, utaulizwa kuingiza namba siri (yenye namba nne). Kisha simu itatoa namba ya utambulisho wa pesa hizo na namba siri kwa mpokeaji huyu tu. Mpokeaji lazima aonyeshe namba ya utambulisho wa pesa na namba siri ili kupokea pesa hizo.

**Uzuri na ubaya wa huduma ya pesa za simu**

**Uliza:**
Unafikiri ni kwa nini huduma ya pesa za simu inaweza kuwa bora zaidi kwako? Kutumia huduma ya pesa za simu kutakusaidiaje?

Hakikisha kwamba hoja zifuatazo zimetajwa kuhusu uzuri na ubaya wa kutumia pesa za simu:

**Uzuri wa pesa za simu**

- Hakuna haja ya kubeba kifurushi cha pesa mfukoni kuzituma kwa akaunti ya pesa za simu ya mtu mwingine kwani zinaweza kuibwa njiani. Unaweza kuhamisha pesa hizo kupitia simu palepale ulipo.
- Shughuli zote za pesa za simu lazima zithibitishwe kwa kutumia namba siri yako ya PIN. Kwa hiyo, usipomwambia yeyote PIN yako, hakuna anayeweza kuiiba au kugusa pesa zako, hata kama umepoteza simu yako au kusahau PIN yako
- Shughuli za pesa za simu zinatekelezwa papo hapo mtandao ukiwa upo
- Inaokoa muda wako na nauri. Hakuna haja ya kuleta pesa taslimu mkononi na kumpokeza mpokeaji. Kama una pesa kwenye akaunti ya simu yako na unataka kutuma pesa kwa mtu fulani, unaweza kuzituma papo hapo kwa kutumia simu bila ya kufasiri kwenda mahali popote
- Kufungua akaunti ya huduma ya pesa za simu ni bure. Lakini, kwa baadhi ya shughuli za huduma ya pesa za simu utalipa ada fulani, kwa mfano ada ya kutuma pesa
- Ni rahisi na laisi kutumia huduma ya pesa za simu ikiwa watu wanaokutumia pesa au kupokea pesa kutoka kwako wamejisajilisha kutumia huduma hii kwenye mtandao kama wako
- Ili kuweka na kutoa pesa kutoka akaunti ya pesa za simu, unatakiwa kwenda kwa ajenti wa huduma ya pesa za simu, na maajenti hawa wanapatikana mahali popote katika eneo lako

**Uliza:**
Unafikiri kutumia huduma ya pesa za simu kuna uzuri na ubaya gani?

Una hofu gani au malalamiko gani juu ya kutumia huduma ya pesa za simu?

Hakikisha kwamba hoja zifuatazo kuhusu ubaya wa kutumia huduma ya pesa za simu zimetajwa:

**Udhaifu wa huduma ya pesa za simu**

- Shida za kuwa na mtandao dhaifu zinaweza kuchelewesha shughuli za pesa za simu. Lakini, ukiwa kwenye eneo ambalo mtandao kawaida huwa na nguvu, shughuli za pesa za simu huwa haraka na bora sana
- Usalama wa PIN, kwani kawaida mume na mke wanaoneshana PIN zao
- Maajenti kuiba kiasi fulani cha pesa za wateja hasa wale wateja wasiojua ada zenyewe za huduma ya pesa za

simu au wasiojua kiasi cha pesa zilizo kwenye simu.

Masharti ya wakimbizi ya kupata kadi za simu ni makali sana

**Eleza:**
Kuna mambo muhimu ya kukumbuka wakati ukitumia huduma ya pesa za simu ili kujiepusha na kuibwa na ajenti au pesa zako kuibwa kutoka akaunti yako ya pesa za simu:

- Usimwambie yeyote PIN yako
- Kamwe usiweke PIN yako na kadi yako ya simu mahali pamoja
- Daima hakikisha kwamba ajenti anakuonyesha orodha ya ada za kila aina ya shughuli ya kutoa na kutuma pesa
- Daima thibitisha kiasi cha pesa na jina la mtu unayemtumia pesa kabla ya kuingiza PIN yako

## Kufahamu haki zako

**Uliza:**
Kama wateja kutoka mashirika ya kifedha mbalimbali (kwa mfano SACCO, Benki, n.k) neno"haki" linamanisha nini kwako? Toa maoni yako kwa darasa zima.

Wambie kwamba haki ni kitu unachostahili kama mteja wa shirika la kifedha.



Chati 09
**Kufahamu haki zako**

**Uliza:**
Unaelewa nini juu ya picha tofauti tofauti unazoziona kwenye chati?

Baada ya wanafunzi kujaribu kutoa majibu, waelezee haki zao ni zipi:

- Kusikilizwa endapo umepata shida (kupata suluhisho): Unaweza kujulisha shirika fulani la kutetea haki, mashirika ya usaidizi, ofisi ya Waziri Mkuu au maafisa wa benki yako kama umepata shida yoyote. Sema wazi shida yako ili iweze kutatuliwa

- Kuhudumiwa kwa heshima: unatakiwa kuhudumiwa kwa heshima wakati wote. Usilazimishwe kusubiri kwa muda mrefu sana au kusubiri ukiwa mahali ambapo huoni faraja. Julisha benki yako kama hujaridhika

- Kupata habari wazi: Hakikisha unapokea habari kamili, za kweli na zinazoeleweka wazi kuhusu shughuli zako za kifedha. Uliza kuonyeshwa ada zote.

- Unaweza kuomba kujua ada zote kamili kwa shilingi badala ya asilimia ambazo kawaida huwa zinachanganya. Uliza kiasi cha pesa zinazohusika (jumla ya pesa zilizotumwa) na kiasi chenyewe cha pesa utakazopokea (baada ya ada zote kukatwa). Usilipe ada yoyote isiyobainishwa kwenye orodha ya ada za benki.

- Kulindwa dhidi ya kushinikizwa na maafisa wa kifedha: Usikubali kusukumwa kujiunga na shirika la kiafedha au kutumia huduma zao bila ya kufahamishwa kikamilifu namna huduma hizo zitakavyokuathiri

- Kuweza kupata pesa zako kwa urahisi: Unafaa kupata pesa zako kila unapozihitaji, na la muhimu zaidi, kulingana na mahitaji yako ya kifedha

- Usiri wa taarifa za mteja: taarifa zako lazima ziwekwe kwa siri

**Kufahamu majukumu yako**

**Uliza:**
Neno majukumu linamaana gani kwako?

Chati 10
**Kufahamu majukumu yako**

Wanafunzi watoe maoni yao kuhusu picha mbalimbali na kueleza kwa kifupi maoni yao pamoja na hoja zifuatazo kama majukumu yao:

- Toa taarifa sahihi na kamili kuhusu wewe na familia yako
- Kuheshimu na kufuata masharti na kanuni za mashirika ya huduma za kifedha
- Kuheshimu mashirika ya kifedha pamoja na wadau wake
- Uaminifu: Usitoe hongo au zawadi yoyote kisiri ili kupewa huduma yoyote. Ufisadi kawaida hushirikisha watu wawili. Usisababishe au kuruhusu ajenti wako kuwa mfisadi
- Ripoti kitendo chochote cha kutendewa dhuluma
- Jaribu kuwa mvumilivu

**Njia za kulalamika na kupata majibu**

Wambie wanafunzi kwamba kufanya malalamiko na kupata majibu ni mojawapo ya haki zao.

Chati 11
**Njia za malalamiko na majibu**

Eleza njia mbalimbali za kufanyia malalamiko na kupata majibu zilizopo katika eneo lao na namna ya kuzitumia.

- Omba namba za simu za bure za kutumia kuomba usaidizi za shirika la kutetea haki, za mashirika ya usaidizi na za shirika la kifedha za malalamiko na majibu, kwa mfano, 0800 210 210 ni namba ya msaada ya shirika la WFP na 0800 323 232 ninamba ya msaada ya UNHCR

- Fikia ofisi za kutoa usaidizi wa kisheria zinazoshughulikia kesi mbalimbali, kwa mfano, malalamiko

- Hudhuria mikutano ya jumuiya na ya eneo lako ili kuripoti malalamiko yako na mambo mengine

- Kwa wale wanaojua kuandika, weka malalamiko yako kweye visanduku vya malalamiko vilivyo katika sehemu mbalimbali na kwa ofisi za mashirika ya ya kutetea haki

- Tumia fomu za usalama zinazopatikana kwa viongozi wa wakimbizi ili kufanya malalamiko au kutoa majibu


- Tumia vibanda vya muda vya kupokea malalamiko katika eneo lako

- Tumia njia mbadala za kufanya malalamiko kama mikutano mingine ya kijumuiya na ya kifedha, rediyo za vijiji, mpiango ya uchunguzi, nk.

**Mwisho wa somo la module 04**

# Kozi pevu





Vikao 7



Vitengo 3

**Kitengo 05**: Shughuli zinazozalisha kipato: Uteuzi, upangaji na uendeshaji
Kipindi 01
**Eleza shughuli inayozalisha kipato (IGA)................................ 33**
Kipindi 02
**Kuchagua shughuli inayozalisha kipato ................................. 38**

**Kitengo 06**: Vitegauchumi
Kipindi 01
**Vitegauchumi ni nini? ..................................................41**
Kipindi 02
**Kupanga biashara yako..................................................43**

**Kitengo 07**: Mikopo, kuweza kudhibiti madeni
Kipindi 01
**Pesa zangu vs pesa za mtu mwingine ................................... 47**
Kipindi 02
**Kulinganisha wakopeshaji................................................ 49**
Kipindi 03
**Mzunguko wa mkopo ..................................................... 53**

## Kazi Zinazoingiza Pesa (KZP)
## Kipindi cha 01

Uliza wanafunzi kufafanua KZP na jaribu kuangaza majibu yanayozingatia yafuatayo:

- Kazi inayoingiza pesa ni biashara inayoendeshwa na mtu binafsi au kikundi cha watu kwa lengo la kupata faida ili kuongeza kipato katika familia

- Ni kazi ambayo mwenye biashara hulenga kuongeza kipato

Jambo muhimu la kusisitiza hapa ni kwamba:

- Wenye KZP wanafaa kuzidisha kiasi cha pesa wanazopata kutoka biashara yao na pia kuongeza kiasi cha pesa wanazotia tena kwenye biashara ili kupanua biashara hiyo

Kitabu cha mazoezi:
urakasa 13
**Mifano ya KZP**

Kitabu cha mazoezi:
urakasa 14
**Sababu za kufaulu au kushindwa**

### Kutambua sababu za kufaulu au kushindwa

Wambie wanafunzi kukaa wawili-wawili, na kila jozi kujadiliana juu ya KZP zao binafsi au zile za familia zao. Jadili KZP ambazo zimefaulu ambazo bado wanazifanya au ambazo wangependa kuzifanya tena, Na KZP ambazo hazijafaulu ambazo hawazifanyi tena.

Sasa uliza wanafunzi kusema hoja walizojadili kwa kuzingatia kufaulu na kushindwa kwake. Majibu wanayotoa yanaweza kuainishwa katika kategoria kuu tano.

### Mambo matano muhimu ya kuzingatia kabla ya kuchagua KZP

Kitabu cha mazoezi:
urakasa 15
**Mambo 5 muhimu kabla ya kuchagua KZP**

Kabla ya kuchagua na kufanya mipango ya kuanzisha KZP fulani, watu wanafaa kuzingatia mambo 5 yafuatayo kwa uangalifu wakati wote:

**1. Maarifa, mbinu na muda**

Ni maarifa na mbinu gani ulizonazo ambazo zaweza kutumika kwa KZP?

Ukiona nafasi ya kuanza KZP lakini huna maarifa na mbinu zinazohitajika, wewe na familia yako mtafanya nini ili kuanzisha KZP?

Usitumie mifano isiyopatikana katika eneo la wanafunzi au inayohitaji pesa nyingi sana. Hakikisha kwamba darasa linajadili nafasi za biashara zinazohusiana na kazi za mashirika yasiyo ya kiserikali, mipango ya serikali na kufanya kazi kwa watu wengine wenye biashara zinazoendelea.

KZP huchukua muda, na unatakiwa kufikiria ikiwa wewe na familia yako mna muda huo wa kutekeleza KZP.
Unaweza kukadiria ni muda gani unaohitajika kufanya baadhi ya mifano ya KZP? Una uhakika kwamba wanafamilia wana muda wa kutekeleza majukumu yao yanapohitajika?

- Muda unaochukuliwa kutengeneza bidhaa au kutoa huduma
- Muda wa kusafiri kununua vitu vinavyohitajika
- Muda wa kusafirisha bidhaa kwenda sokoni, au kwenda mahali ambapo unatoa huduma hiyo
- Muda wa kufanya KZP zinginezo

**2. Kutangaza bidhaa na kutafuta**

**Sema:**
Sasa tunafikiri tuna maarifa, mbinu na muda vinavyohitajika kufanya KZP. Lakini kabla ya kujaribu kuuza bidhaa au huduma, lazima tuhakikishe kwamba wateja wa kutosha watahitaji tunachouza.
Kuna maswali muhimu ambayo lazima tujiulize wakati tukifikiria jambo hili, na tutayajadili pamoja.

**Uliza:**
Tuna uhakika kwamba bidhaa au huduma ambayo tunajua namna ya kuitoa ni kitu ambacho watu wengi watakihitaji na kukinunua? Je, tumefanya uchunguzi kuhusu kile watu wanachonunua sasa?

Kitu au huduma ambavyo darasa litatoa huenda havitavutia kama bidhaa au huduma zingine zinazofanana navyo. Kwa mfano, nguo zinazotengenezwa hapa zinaweza kutovutia kama nguo zinazotoka nje ya nchi na kuzwa kwa bei sawa. Je, nina uwezo wa kutoa kitu au huduma katika mahali ambapo wateja wanataka kukinunua? Je, nina uwezo wa kujisafirisha na kusafirisha vituy vyangu kwenda sehemu hiyo, na kuhakikisha kwamba wateja wana fursa ya kununua kutoka kwangu?

Ili KZP kufaulu, vitu na huduma vinatakiwa kuuzwa katika sehemu ambayo wateja wanataka kuvinunua. Sehemu hii inaweza kuwa sehemu ambayo wateja wanaishi au kwenye soko la kila wiki. Wauzaji na familia zao wanafaa kuwa na muda, na kuwa na uwezo wa kusafiri kwenda sehemu wanayotaka kuuza vitu na huduma?

Je, watu wengi wanajua namna ya kutengeneza vitu ninavyotaka kuuza katika KZP yangu? Kama ni kweli, je, ninafikiri nitaweza kuvitengeneza vyema kuliko wengine, ndipo niweze kufaulu?

Watu binafsi wa makundi ya watu wanaweza kuamua kuwekeza kwenye KZP kwa sababu wanaona watu wengine wakifanya hivyo. Lakini, mashindano katika biashara yanasababisha uamuzi mbaya wa kibiashara kwa kila mtu kwani bidhaa zitakuwa nyingi kuliko wanunuaji?

Kukiwa na watu wengi wanaofanya biashara fulani, biashara mpya zinafaa kuanzishwa na mtu mwenye mawazo mapya na yaliyo bora zaidi ambayo yanaweza kushindana vyema na biashara zingine. Kuwa na bidhaa mpya na iliyo bora kuliko zingine inaleta faida.

**Uliza:**
Ni mambo gani mengine unayofaa kuzingatia kabla ya kuamua ni biashara gani utakayoanzisha?

Ruhusu baadhi ya wanafunzi kutoa majibu yao kabla hujatoa majibu yafuatayo:

Vyombo na zana:

- Ni zana na vyombo gani ambavyo vitahitajika?
- Nitahitaji vingapi kwa kila?
- Vinauzwa pesa ngapi?
- Nitavinunua wapi?
- Ninaweza kuvipangisha au kuvikodi?
- Vyombo vitahitaji marekebisho?
- Nani atafanya matengenezo?

Vifaa na Malighafi:

- Ni vifaa gani na malighafi zingine ambavyo vitahitajika?
- Nitahitaji vingapi na vya kiwango gani?
- Vitahitaji pesa ngapi?
- Vifaa hivi nitavipata hapa katika eneo langu?
- Nitasafirishaje vifaa hivi kwenda sehemu ya kutengenezea bidhaa?

Njia ya kutengeneza mbidhaa na mahali:

- Nitatumia mbinu gani ya kutengeneza bidhaa?
- Nina uzoefu wa kutumia mbinu hiyo?
- Ninajua namna ya kutatua shida yoyote inayoweza kutokea?
- Ninajua mahali pa kupata usaidizi?
- Shughuli hizi zitatendeka wapi?
- Mahali penyewe ni mwafaka?
- Kama nitahitaji kutumia nguvu za umeme, utapatikana?

Wafanyakazi:

- Shughuli hii inahitaji muda gani?
- Je, mimi na familia yangu tutaweza kupata muda huo wote?
- Nitahitaji wafanyakazi wowote wenye ujuzi maalumu?
- Kama ndiyo, watu hao wanapatikana?
- Kama ndiyo, watahitaji pesa ngapi?

**3. Faida ya biashara hii**

Mauzo yanayotarajiwa, gharama ya shughuli za biashara za kila siku na pesa za kuanzisha biashara:

Ili biashara kuleta faida, itabidi kutoa gharama ya kazi kutoka pesa inazoingiza, na tofauti, ili kuwa faida, isiwe deni. Kuna aina mbili za gharama za kufikiria:

Hiki ni kiasi cha pesa unazohitaji ilikuanzisha biashhara:
Hivi ni vitu unavyohitaji kununua mara moja, ambavyo vinazidi kutumika katika mchakato wa kuzalisha mali mara kwa mara.

Gharama ya kazi za kila siku:
Hiki ni kiasi cha pesa unachohitaji kuendeleza biashara baada ya kuianzisha. Kiasi hiki kinahusiana na mchakato wa kuzidi kuzalisha mali, ambao ni muda unaochukuliwa kwa bidhaa fulani kutengenezwa na kuuzwa. Kwa shughuli za kilimo na ufugaji, mchakato huu utachukua miezi kadhaa lakini kwa biashara ndogondogo mchakato unaweza kuchukua hata siku moja tu.

Lazima uhakikishe kwamba una pesa za kutosha kugharimia gharama za aina zote mbili. Mwalimu achague biashara

moja miongoni mwa zile zilizotajwa na wanafunzi kama mfano na kujadiliana na darasa zima juu ya makadirio ya gharama ya kuanzisha biashara, gharama ya kuendesha biashara kila mwezi na mauzo ya kila mwezi. Mwishoni, ithibitishwe ikiwa biashara hiyo itaweza kulipa gharama ya kila mwezi na pia kuacha faida fulani mwishoni mwa mwezi.

**Sema:**
Kuna aina tatu za gharama ambazo zinatakiwa kulipwa mara kwa mara na kwamba pesa za kulipia gharama hizi lazima ziwekwe kando kabla ya pesa zozote kuchukuliwa na familia.

Hizi ni pamoja na:
- Kununua mali mpya kila siku badala ya kusubiri hadi mali karibu kumalizika (kama ni biashara yenye mauzo ya kila siku)
- Kulipa mikopo na madeni
- Kuhifadhi pesa ili kugharimia gharama iliyoanzisha biashara, kuwekeza katika kupanua biashara hiyo au kuwekeza kwenye biashara nyingine ya familia

**4. Vyanzo vya rasilimali**

**Sema:**
Katika sehemu hii tutajadili vyanzo vya pesa za kuanzisha biashara, na kujadili pia uzuri na ubaya wa kila chanzo

Pesa ulizohifadhi ndizo pesa salama zaidi za kutumia kuanzisha biashara:

- Biashara yako isipofaulu, hutakuwa na deni la mtu yeyote
- Hutegemei mtu mwingine yeyote wakati wa kufanya uamuzi
- Unaamua mwenyewe namna ya kutumia faida kutoka biashara
- Haihitaji kutoa mali kama usalama
- Ukipata dharura na unahitaji kutumia pesa ulizohifadhi hazitakuwepo
- Inaweza kuchukua muda mrefu kuhifadhi kiasi cha pesa zinazohitajika

**Familia**

Kama hijahifadhi kiasi cha pesa za kutosha, unaweza kutumia mchango wa familia. Familia inaweza kushika dau katika biashara hiyo au. Wanawza kukukopesha pesa hizo kwa bure au kwa kutoza ribaa fulani.

- Biashara yako isipofaulu, jamaa yako hatakushinikiza kulipa deni lake
- Kama utatoa uamuzi pamoja na mwingine, mtu huyu atakuwa jamaa yako badala ya mtu kutoka nje ya familia
- Kama ni lazima kutumia kiasi fulani kutoka faida ya blashara kulipa pesa ulizotumia kuanzisha biashara, huwa unarudisha pesa hizo katika familia
- Haihitaji kutoa mali kama usalama
- Huenda hutaki kushirikisha familia kwenye biashara yako, kwa hiyo unaweza kuamua kupata mkopo kutoka shirika la kifedha au kutoka mahali pengine nje na familia
- Biashara isipofaulu, kupoteza pesa za familia kunaweza kuleta uhasama
- Jamaa yako wanaweza kudai vitu na huduma vya bure au kwa bei ndogo iwapo wamekukopesha pesa

### Mikopo kutoka mashirika ya hifadhi na mikopo

Mikopo hii ina utata kuliko pesa za familia au marafiki, lakini pia ina uzuri mkubwa

- Bado unajitegemea wakati wa kufanya uamuzi
- Bado unajitegemea katika uamuzi wa kutumia faida ya biashara
- Ni rahisikupata
- Haihitaji usalama
- Unapata ushauri na usaidizi kutoka wanachama
- Unapata sehemu ya faida kutoka shirika la hihadhi na mikopo
- Masharti ya kulipa mkopo si makali na wanachama wanajitahidi kufahamu shida yako
- Kipindi cha kulipa mkopo cha shirika (miezi 3) ni kifupi sana
- Mikopo kutoka mashirika haya si mikubwa
- Biashara isipofaulu na ukashindwa kulipa mkopo utapoteza heshima katika eneo lako
- Kama shirika linatoza ribaa isiyopunguka wakati ukilipa, ribaa inaweza kuwa kubwa mno

### Mikopo kutoka benki

Mikopo hii ndiyo ina utata zaidi lakini pia ina uzuri mwingi kwa biashara zilizokwisha imarika (zisizoanza tu)

- Mikopo inalipwa kwa kipindi kirefu kuliko ile ya mashirika ya mikopo
- Zinatoa mikopo mikubwa
- Tawi la benki laweza kuwa mbali na unahitajika kusafiri huko mara kadhaa
- Hatua za kupata mkopo ni ngumu na huchukua muda mrefu
- Ratiba ya kulipamkopo haibadiliki na inaweza kutolingana na namna biashara inavyoingiza pesa
- Kupata mkopo unahitaji mali ya usalama wa mkopo, jambo linalohatarisha mali yako ukishindwa kulipa mkopo
- Ushirikiano baina yako na benki ni wa rasmi na hauna urafiki
- Baadhi ya benki hazisikilizi na kuelewa shida unazokumbana nazo kwenye biashara na ambazo haziepukikani

### Mikopo kutoka wakopeshaji

- Ni rahisi kupata na kwa muda mfupi
- Zinapatikana katina eneo lako
- Mikopo inaweza kulipwa kwa muda mrefukuliko zile za mashirika ya mikopo
- Zinazota ribaa kubwa sana kuliko wengine wote
- Zinahitaji mali ya usalama. Wakati mwingi watu hupoteza mali ya usalama kwa sababu ya ile ribaa kubwa sana

### 5. Kipato cha familia

Sehemu hii inahusu kuhakikisha kwamba biashara uliyochagua ndiyo inafaa zaidi kwa familia yako. Sababu moja ya kutofaulu kwa biashara ni kulazimika kutoa pesa kwenye biashara kugharimia mahitaji ya familia. Familia zisizo na kipato kinachotegemewa zinafaa kuzingatia biashara zinazohitaji pesa ndogo kuanzisha na ambazo zinaingiza pesa haraka na kila siku, kwa mfano, kununua na kuuza vitu ambavyo watu wanavitumia kila siku kama kupika chakula cha kuuza.

Kwa kifupi, mtu anafaa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo kabla ya kuchagua biashara ya kufanya:

- Ujuzi, mbinu na muda: Je, nina ujuzi na mbinu za kutekelezea biashara na nina muda wa kufanya, kutawala au kuisimamia?
- Soko na wateja: Kuna watu wa kutosha watakaonunua vitu au huduma?
- Kiasi cha faida: Biashara ina uwezo wa kuleta faida?
- Chanzo cha pesa: nina pesa za kutosha za kuanza biashara na kuiendesha kila siku?
- Kipato cha familia: Pesa kutoka biashara, zikiongezwa kwenye pesa zingine katika familia, zitatosha kugharimia mahitaji ya familia?




Kazi ya nyumbani:
**Uliza wanafunzi kufikiria biashara wanayopenda baada ya kipindi hiki, kila mtu darasani aanze kuzingatia biashara moja ambayo ameichagua**

Katika kipindi kifuatacho kila mwanafunzi awe tayari kujadili biashara aliyoichagua. Kila mtu awe tayari kujadili kwa dakika chache akielezea:

- Kwa nini ameamua kuwa na ujuzi na mbinu za kufanyia biashara hiyo
- Ni wapi soko na wateja wake walipo, na wapi atauza vitu au huduma zake
- Amekadiria kiasi gani cha pesa za kuanzisha biashara pamoja na kiasi cha pesa za kuendesha biashara kila siku mpaka biashara itakapoanza kuleta faida
- Amekadiria kiasi gani cha pesa zinatazoingizwa na biashara kila mwezi, gharama ya kila mwezi na faida ya kila mwezi (faida ya jumla na faida halisi)
- Kwa nini anafikiri chaguo lake la biashara ni mwafaka kulingana na uwezo wa kuwekeza na kipato vya familia yake

## Kipindi 2

Hadi sasa, kila mwanafunzi ameandaa wasilisho lake la kibiashara, linalozingatia yale mambo 5 muhimu.

Kila mwanafunzi anawasilisha na kujibu maswali na kuruhusu darasa kujadili wazo lake. Hakikisha kwamba mjadala unatoa mawazo ya kusaidia mtu huyu, na watu wakihisi kwamba mtu huyu hajahakiki vyema biashara yake, au familia yake vyema. Wanaweza kumsaidia. Usiwaruhusu kumvuja moyo mwenzao, bali, msaidie kila mtu ili ahisi kwamba anapiga hatua mbele wakati wa mijadala hii.


Hakikisha kwamba kila mwanafunzi anazingatia yale mambo 5 katika wasilisho lake:

- Kwa nini wameamua kuwa na ujuzi na mbinu vya kufanyia biashara yao?
- Wateja wao ni kina nani na wanapatikana wapi ambako watawauzia vitu na huduma?
- Makadirio yao ya faida halisi kutoka biashara hiyo kwa kuzingatia pesa za kuanzisha biashara, gharama ya kuendesha biashara na makadirio ya kipato
- Namna watakavyopata pesa zinazohi-

tajika kuanzisha biashara hiyo

- Kama wanafikiri biashara hiyo itatoa mchango wapesa za kutosha kwenye pesa za kugharimia mahitaji ya familia

Tumia hayo mambo 5 kuongoza mjadala wa kila mwanafunzi kisha wape alama.




Mfano wa 07
**Duka la Aisha**

## Mipango ya kuanzisha biashara


Kila mwanafunzi sasa ataanza kuzingatia mipango ya kuanzisha biashara yake wakati ukiwapa maswali ya mwongozo ambayo watayajadili. Chukua dakika chache kueleza kila swali, na wanafunzi katika jozi zao watasaidiana kujibu maswali hayo.

Maswali ya mwongozo (yapitie yote):

- Wewe au mtu mwingine atakayeshughulika kwenye biashara, mtahitaji ujuzi na mbinu zaidi? Kama ndiyo, mtajifunzaje mbinu hizo?
- Wateja wako lengwa wana mahitaji gani hasa, na utawajulishaje kwamba una kitu au huduma itakayowaridhisha?
- Kama utahitaji mahali pa kuuzia vitu vyako, je, umetafuta hayo mahali tayari na pia umetayarisha njia za kusafirisha bidhaa?
- Utaanzisha biashara yako lini?? Ni muhimu kuanza wakati mahususi katika mwaka, na kama ndiyo, utakuwa tayari?
- Unahitaji vifaa na vyombo gani, na utavipata kutoka wapi?
- Umehesabu pesa ngapi za kuanzisha biashara na pesa ngapi za kuiendesha kwa angalau miezi 3?
- Umehifadhi pesa hizo tayari? Kama hapana, utazihifadhi kwanza au utapata mkopo?
- Kama utapata mkopo, una uhakika kwamba ni wazo bora kukopa kulingana
- Na aina ya biashara yako pamoja na hali ya kifedha ya famila yako?
- Kama utahitaji nguvu za umeme, maji au nishati ili kufanyia biashara yako, je, vipo?
- Umekwisha pata idhini na leseni kutoka mamlaka mbalimbali?



Kitabu cha mazoezi:
urakasa 16
**Mipango ya kuanzisha biashara**



Wanafunzi watayarishe chati nyepesi inayoonyesha mambo yote wanayotarajia kufanya kabla ya kuanzisha biashara kumaliza angalau miezi 6 baada ya kupata pesa za kuanzisha biashara.

Uliza mwanafunzi mmoja ambaye amekuwa makini katika kipindi afafanue hatua atakazochukua na kujaza karatasiya kielelezo kama mfano kwa darasa zima. Hakikisha kwamba kila mwanafunzi ameelewa kabla hujaendelea.

Wambie wanafunzi kuzingatia yafuatayo kwa ajili ya biashara zao:

- Jina la biashara: Taja biashara ambayo unafanya au unapanga kufanya, kwa mfano, kutengeneza Chapatti
- Chanzo cha pesa: Bainisha mahali ambapo pesa za kufanya biashara zitatoka
- Bidhaa na/au huduma: bidhaa zitakuwa vitu gani au huduma gani unavyotaka kutoa kwa wateja wako?
- Wateja wa bidhaa/huduma: Bainisha wateja wako ni kina nani
- Washindani wako: Fahamu ni kina nani wanaofanya biashara kama yako? Udhaifu na nguzu zao ni vipi? Ni kitu gani utakachofanya bora zaidi kuliko wao?
- Kudadisi uwanja wa biashara yako: Fahamu uwanja wa biashara ambamo unataka kufanyia biashara yako (ni uwanja wa kilimo au si wa kilimo). Uwanja huo unakumbwa na madhara gani na pia unakuwa na faida gani?
- Kutathmini wateja: idadi ya wateja imekuwaje katika kipindi cha nyuma (wanaongezeka au wanapunguka), wateja wanatoka tu eneo hilo au pia wanatoka nje?
- Kudadisi chanzo cha vifaa: Vitu vya kufanyia biashara yako vitatoka wapi (bidhaa au mbegu au mbolea)?
- Usimamizi wa biashara: Nani atakuwa msimamizi kamili wa biashara hiyo?










**Mwisho wa somo la 05**

## Kuwekeza ni nini?
## Kipindi 1

**Sema:**
Kuwekeza ni kutumia pesa kwa namna ambayo inazifanya kuongezeka. Mtu anaweza kuwekeza katika vitu kama kununua mali au ufugaji (ngombe, nguruwe, mbuzi), ardhi (kwa mfano kujenga nyumba za kupangisha, kujenga majengo ya kibiashara), kuanzisha biashara (kuuza sokoni, kuuza duka, bodaboda) au kununua hisa na bondi ambavyo vinakuletea faida.

Watu huwekeza ili:

- Kupata pesa za kutosha kugharimia mahitaji yao yote
- Kuwezesha pesa zao kuongezeka bila wao kushughulika na kuongeza kipato kwa matumizi ya siku za mbele, pesa ambazo mtu anaweza kuziwekeza tena kwingineko
- Ukiamua kula pesa zako, kwa mfano, kununua televisheni, pesa zitakuwa zimekwenda bila ya kukusaidia kupata pesa zaidi siku za mbele
- Kujenga utajiri na usalama wa kimaisha
- Kuongeza uwezo wa kuzidisha kipato
- Kuanzisha biashara zinakazo zidi kuingiza pesa uzeeni
- Kuanzisha ajira kwa mtumwenyewe na kwa familia yake

## Mifano ya uwekezaji ni kama ipi?

Wape nafasi wanafunzi kutoa mifano kabla hujataja yafuatayo:

- Kuanzisha biashara ya rejareja
- Kununua mashine
- Kujenga majengo
- Kufuga kuku
- Kununua hisa kwenye shirika la hifadhi na mikopo
- Kununua mifugo

Chati 12
**Njia mbalimbali za kuwekeza**

Eleza njia mbalimbali za kuwekeza:

**Biashara**

Biashara zinaweza kuanzishwa kutoa huduma, kutengeneza bidhaa na kuziuza nje ya nchi. Watu wengi wanauza huduma na bidhaa kupitia maduka ya rejareja na maduka makubwa ya kujumlisha. Aina za kawaida za biashara ni pamoja na saluni, bodaboda, shule, hoteli, mikahawa, maduka ya rejaleja na ya kujumlisha, nk.

**Kilimo**

Nchini Uganda, kuna nafasi nyingi za kuwekeza katika kilimo kwa njia ya kuzalisha mazao, kuyatengeneza na kuyauza nje ya nchi. Uwekezaji unaweza kufanyika kwa mfano katika kufuga kuku, nguruwe, kuvua samaki, kupanda miti, kupanda mimea (kama mahindi, kahawa au ndizi), kilimo cha matunda, kuyatengeneza na kuyapakia.

**Rasilimali**

Kuwekeza katika majengo au ardhi kunaleta faida kwa kutegemea hali ya


soko. Kabla ya kuwekeza, ni muhimu kutathmini thamani, mazingira, gharama na soko la aina ya majengo au ardhi unayotaka kununua.

**Kuwekeza benkini**

Unapoweka pesa benkini kwa makubaliano ya kipindi fulani na kupewa cheti, huwa umekopesha benki pesa zako na unapewa ribaa. Unawekeza benkini kwa kuweka pesa kwenye akaunti ya ribaa iliyofunguliwa kwako na benki.

Utapewa ushahidi kwamba umewekeza na utapokea ribaa kila baada ya kipindi fulani au mara moja mwishoni mwa kipindi cha makubaliano. Ni sharti benki ikulipe ribaa iliyobainishwa.

**Kanuni bora za uwekezaji**



Kazi ya vikundi:
**Unda vikundi vya watu 2-3. Kila kikundi kiandike kanuni bora za kuzingatia wakati wa kuwekeza**

Wanafunzi wape dakika 5 kukamilisha zoezi hili. Uliza kila kikundi kusema majibu yake kwa sauti. Jadili mapendekezo yao kwa kusema yafuatayo:

- Tayarisha bajeti kabla ya kuwekeza. Andika pesa zinazotarajiwa, gharama za kila siku na pesa za matumizi ya dharura kwa wiki kadhaa au miezi, na uone kiasi cha pesa zinazobaki ili kuzihifadhi au kuziwekeza kwingineko
- Baada ya kuandaa bajeti, fanya mipango kabla hujawekeza kwenye biashara yako. Yaani, fahamu ni muda gani, pesa ngapi na nguzu ambavyo uwekezaji huo utachukua, na lini utaweza kutekeleza uwekezaji huo
- Pata ushauri kutoka wataalamu kabla ya kuwekeza
- Hifadhi pesa (weka pesa kando) kabla ya kuwekeza pesa mahali fulani
- Anza kwa kuwekeza pesa ndogo ndogo ili hatari ya kupoteza pesa iwe ndogo mwanzoni. Utakavyozidi kupata faida ndivyo utakavyozidi kuwekeza kwenye biashara kubwa zaidi
- Wekeza kwenye mahali ambako biashara na pesa zako vinaongezeka. Ukiwekeza katika kufuga kuku, kuku watataga mayai ya kuuza
- Weka kumbukumbu. Andika kiasi cha pesa ulizowekeza, aina ya biashara, na ikiwa unapata faida kutoka biashara hiyo

**Ujumbe wa msingi:**
Wekeza kwa busara ili biashara yako ipate kukua. Fikiria kabla ya kuchukua hatua!




Kazi ya nyumbani:
**Uliza kila mwanafunzi kuboresha mpango wake wa kibiashara au wa uwekezaji**

Wambie wanafunzi kupekua ukurasa wa 10 na kurudia zoezi lile la 'Kufanya mipango ya biashara' (Somo la 5) na kurejelea maswali yaliyo kwenye kitabu cha mazoezi, ukurasa wa 10 'maswali ya kuuliza kabla ya kuwekeza'.

Wanafunzi wahakikishe kwamba mpango wao una uhalisi na unaweza kutekelezwa kulingana na hali yao ilivyo sasa, na kwamba wana uwezo wa kuutekeleza wao wenyewe. La sivyo, itawabidi kuufanyia mageuzo na kufikiria tena mpango wao.

## Kipindi 2

Anza kipindi hiki kwa kuuliza wanafunzi kujadili zoezi la nyumbani. Kila mwanafunzi awasilishe mpango wake wa kibiashara au wa uwekezaji mbele ya wenzake. Hakikisha kwamba wanafunzi wengine wanatoa mawazo na ushauri kwa mwenzao na kumwongoza katika kufanya uamizi mzuri.

Jadili:
**Uliza kila mwanafunzi kujiunga na mwenzake ili kujibu swali: kwa nini kuwekeza ni muhimu?**

Wape nafasi wanafunzi wawili-wawili kujadili kwa dakika 5. Wambie kuwasilisha majibu yao mbele ya darasa. Hakikisha kwamba wanafunzi wametaja majibu yafuatayo:

- Biashara yako inasitawi
- Ni njia ya kuhifadhi pesa
- Pesa unazopata kutoka biashara zinaweza kuwa nyingi zaidi kuliko pesa ulizowekeza humo

**Uliza:**
Hatari ni nini katika muktadha wa uwekezaji? Wape nafasi wanafunzi kutoa majibu kabla hujatoa ufafanuzi rasmi:

- Hatari ni uwezekano wa kupoteza pesa katika biashara au kupata faida tofauti za ile uliyotarajiaon

- Hatari pia ni uwezekano wa kupoteza sehemu au jumla ya pesa ulizowekeza. Kwa mfano, kuwekeza kwenye mifugo kuna hatari pale wanyama wako wakiambukizwa na maradhi fulani, unaweza kupoteza wanyama wote na kushindwa kupata tena pesa ulizokuwa nazo mwanzoni kabla ya kununua mifugo

**Uliza:**
Kuna hatari zipi unapowekeza? Wape nafasi wanafunzi kujadiliana wawili-wawili kwa dakika 5. Uliza wanafunzi kujadili majibu yao kwa sauti. Hakikisha kwamba wanafunzi wametaja majibu yafuatayo.

- Unahitaji pesa ili kuwekeza, na kwa hiyo ni vigumu kwa baadhi ya watu kuanzisha biashara yao ya kwanza

- Unahitaji muda na uvumilivu. Hakuna biashara inayoleta utajiri kwa haraka sana

- Kuwekeza kunaweza kuwa na hatari. Kuna hatari ya kupoteza pesa zote biashara isipofaulu.

**Uliza:**
Unawezaje kudhibiti hatari katika biashara? Wape wanafunzi wawili-wawili nafasi ya kujadiliana kwa dakika 5. Uliza wanafunzi kusema majibu yao kwa sauti. Hakikisha kwamba wanafunzi wametaja majibu yafuatayo:

- Fanya mipango vizuri na mapema
- Anza na biashara ndogo ndogo
- Tafuta ushauri kutoka watu waliowahi kufanya biashara kama hiyo usiwekeze pesa zako zote katika biashara moja (usiweke mayai yote kikapu kimoja)



Shuguli:
**Simulia biashara uliyowahi!**

**Sema:**
Sasa tutaambiana tajriba zetu za kuwekeza. Tembea darasani na mwambie mtu mmoja tajriba yako nzuri na mbaya kuhusu biashara uliyofanya na kitu ulichojifunza kutoka biashara hiyo.

Baada ya kuambiana tajriba zenu, tembea tena na umwambie mtu mwingine tajriba zako, kisha endelea kufanya hivyo na mtu mwingine.

Baada ya dakika 5, chagua baadhi ya wanafunzi kuema baadhi ya tajriba ambazo wamezisikiliza kutoka kwa wenzao, na walichojufunza kutoka hadithi hizo.

**Ujumbe wa msingi:**
Assess the risks and rewards of each venture before investing your money.



Mfano 08
Ronald anawekeza kwenye shamba lake

**Maswali ya kuuliza kabla hujawekeza**

Wambie wanafunzi kufikiria ni maswali gani ambayo ni muhimu kuyauliza kabla ya kuamua kuwekeza au kutowekeza. Wafikirie mambo ambayo yameshughulikiwa kuhusu uwekezaji hadi sasa.



Chati 13
**Maswali ya kuuliza**

- Uwekezaji unatekelezwaje? Unafahamu biashara hiyo vizuri kiasi kwamba unaweza kuifafanulia mtu mwingine?

- Malengo yako ni yapi? Je, unatafuta usalama wa kifedha, kipato au kupanua biashara? Au ni yote mawili—kupanua biashara na kipato?

- Biashara hii ina hatari gani? Uko tayari kuzikabiri hatari hizo?

- Unatarajia kupatakiasi gani cha pesa kutoka biashara hii? Je, hicho kiasi kinaweza kupatikana?

- Unapanga kuwekeza kumalizamuda gani? Ni muda mfupi, mrefu kidogo au mrefu sana?

- Kuanunua, kuweka na kuuza bidhaa kutahitaji gharama gani? Je, utalipa kodi kutoka pesa utakazopata?

- Ni biashara zipi ulizo nazo tayari? Biashara hii inalinganaje na hizo biashara zingine? Itageuzaje mkao wa rasilimali zako?

## Umuhimu wa kuwa na biashara mbalimbali


**Sema:**

- Biashara mbalimbali hazitoi faida kubwa wakati sawa
- Biashara mbalimbali zinaathirika kwa namna tofauti na matukio ya duniani, mabadiliko ya ribaa na mambo mengine katika uchumi
- Wakati biashara moja imeshuka, nyingine inaweza kutoa faida kubwa
- Kuwa na biashara za aina mbalimbali kunaweza kukusaidia kusawazisha kipato chako





Chati 14
**Umuhimu wa kuwekeza mahali mbalimbali**



**Muhtasari wa somo:**

- Uwekezaji ni kitendo cha kuweka pesa kwenye shughuli fulani ukitarajia pesa hizo kuongezeka
- Kuwekeza kunaweza kufanyika katika kununua mali, kwa mfano, mifugo (ng'ombe, mbuzi, nguruwe), nyumba (nyumba za kupangisha), biashara (kuuza sokoni, kuuza duka, bodaboda) na vinakupa faida.



Sababu za kuwekeza?

- Kujenga utajiri
- Kuongeza uwezo wa kupata pesa zaidi
- Kujiajiri na kuajiri familia na watu wengine



Njia mbalimbali za kuwekeza:

- Biashara ya kilimo
- Kuuza bidhaa
- Kutoa huduma
- Usafiri
- Kuweka pesa benkini kwenye akaunti ya ribaa

Vyanzo vya pesa za kuwekeza:

- Pesa ulizohifadhi
- Mikopo
- Misaada
- Kuwekeza faida tena



Njia za kupunguza hatari:

- Kila biashara inakumbwa na hatari fulani. Kuna hatari ya kupoteza pesa, kuibiwa, kutumiwa vibaya, kuangamia au kuharibika

- Fuatilia biashara zako vizuri ili kuhakikisha hazipotezi pesa na muda

- Kuwekeza mahali mbalimbali: Usiweke mayai yako yote kwenye kikapu kimoja! Uwekezaji mahali mbalimbali hupunguza hatari kwa kuifanya hatari kumezwa na kufishwa na biashara mbalimbali

- Kuna nafasi ya kupata faida kubwa pale ambapo hatari ni kubwa, na kinyume ni sawa



**Mwisho wa somo la 06**

## Tofauti kati ya pesa zangu na pesa za mtu mwingine
### Kipindi 1



Kazi:
**Fanya onyesho ambapo wewe ni mteja anayepokea pesa kutoka benki na kwa mkopeshaji**

**Sema:**
Naomba watu wawili waje mbele. Mmoja wenu atakuwa afisa wa benki na mwingine atakuwa mkopeshaji.

Kwa kila mmoja kati ya watu wawili hao, toa kadi iliyoandikwa kiasi cha UGX 10,000 kwa mwandiko mkubwa ziweze kusomwa na darasa zima.

Mwambie afisa wa benki: Ningependa kuchukua UGX 10,000 kutoka akaunti yangu ya hifadhi!

Onyesha darasa zima kwa furaha, hizo UGX 10,000 ulizopewa na afisa wa benki.

Mwambie mkopeshaji: Nataka UGX 10,000 haraka iwezekanavyo. Nina dharura!

Inua hizo UGX 10,000 ulizokopa kwa mkopeshaji ili darasa zima wazione.

Inua kadi zote mbili, moja katika kila mkono. Waulize wanafunzi:

Kuna tofauti gani kati ya hizi UGX 10,000 na hizi UGX 10,0000 zingine? (UGX 10,000 za kwanza ni pesa zangu nilizohifadhi; na UGX 10,000 za pili ni pesa za mkopeshaji na ni mkopo. Atazitoza ribaa na ni lazima nimlipe tena peza zake).

**Mkopo ni nini?**

Wape nafasi baadhi ya wanafunzi kujibu kabla hujatoa jibu lifuatalo:

Mkopo ni pesa ambazo mkopaji anaweza kutumia kwa muda. Baada ya kipindi fulani, pesa hizo zinarudishwa kule zilikokopwa, kawaida kwa kuwekwa ribaa au ada fulani.

Kwa nini watu wanakopa pesa:

- Kuwekeza
- Kugharimia dharura fulani
- Kuzitumia kununua kitu fulani ambacho hawana pesa za kutosha kukigharimia

**Uliza:**
Eleza sababu zilizokufanya kukopa pesa?

Nani amewahi kukopa pesa kwa sababu mbali na hizi? Tafadhali twambie ulinganifu uliopo baina ya aina zote tatu za mkopo. Kuna tofauti gani?

Hakikisha kwamba wanataja yafuatayo:

- Mikopo inayotumika kuwekeza inazalisha pesa mpya kwa mkopaji

- Mikopo inayotumika kugharimia dharura na matumizi ya kibinafsi haizai pesa mpya na lazima ilipwe kutokana na vyanzo vingine vya pesa. Jitahidi kuhifadhi pesa na kujiepusha na kukopa pesa kugharimia mambo kama haya

**Uliza:**
Kuna tofauti gani kati ya kutumia pesa

zako na kutumia pesa za mkopo?

Wape nafasi baadhi ya wanafunzi kujibu kabla hujatoa jibu lifuatalo.

- Unaweka ribaa kwenye mkopo
- Mkopo una masharti kadhaa kwa mkopaji, kama kulipa pesa hizo tena na kuweka ribaa, na wakati mwingine unatakiwa kuwa mwanachama wa kikundi fulani
- Una uhuru zaidi unapotumia pesa zako
- Ukipata mkopo, unapata kiasi kikubwa zaidi cha pesa kuliko kile unachoweza kuwa nacho ukitumia pesa zako
- Kupata mkopo kunakuwezesha kupata pesa kwa haraka kuliko unapotegemea uwezo wako wa kuhifadhi kiasi kidogo kidogo

**Tofauti kati ya mkopo mzuri na mkopo mbaya**

**Sema:**
Kuna njia tofauti tofauti za kupata pesa za kufanya biashara yako. Baadhi ya watu hutumia pesa zao, wakiwekeza faida tena, hatuua kwa hatua. Wengie wanapata mkopo ili kuanza au kupanua biashara. Nitasoma visa viwili vinavyotuonyesha njia mbili za kukuza biashara. Sikilizeni na kujiuliza ni nani kati ya wanawake hawa wawili ndiye unajihusisha naye:



Mfano wa 09
**Kisa cha Rose**



Mfano wa 10
**Kisa cha Mercy**

**Uliza:**
Unatakiwa kufahamu mambo gani kabla ya kukopa pesa?

Wape nafasi baadhi ya wanafunzi kujibu kabla hujatoa jibu lifuatalo:

- Kiasi cha pesa za mkopo unazolipa mkiwemo kiasi ulichokopa, ribaa na ada
- Mahali ambapo pesa za kulipa mkopo zitatoka
- Lini utapata mkopo huo (itakuwa kabla unataka kuutumia?)
- Kwamba rasilimali utakayonunua ukitumia huo mkopo itakuwepo mwishoni mwa kipindi cha kulipa mkopo na kuendelea kukupa kipato
- Kwamba bei unayouzia bidhaa zilizonunuliwa kwa kutumia ule mkopo ni ya juu kiasi kwamba itakuwezesha kulipa mkopo na pia kupata faida

## Mambo ya kuzingatia kabla ya kupata mkopo

Wape nafasi baadhi ya wanafunzi kujibu kabla hujatoa jibu lifuatalo:

- Ukubwa wa mkopo
- Kipindi cha kulipa mkopo
- Ribaa ya mkopo
- Ada za mkopo
- Muda wa kujitayarisha kabla ya kuanza kulipa
- Ratiba ya kulipia mkopo
- Costs of borrowing

**Sema:**
Kama umewahi kupata mkopo, unajua kwamba gharama za moja kwa moja ni zile pesa unazolipa kwa mkopeshaji ili kupata mkopo. Hizi ni pamoja na ribaa,

ada ya mkopo na ada za kuchelewa kulipa. Tusizisahau kwani lazima tuhakikishe kwamba tunaweka kando pesa za kutosha kila wiki au kila mwezi ili kufanya malipo haya. Lakini wakati mwingi hatujui ada za ziada tunazotakiwa kulipa kwa sababu ya kuwa na mkopo huo, kama kutohudumia wateja au pesa tunazolipa kusafiri kwenda kuhudhuria mikutano au kwenda benkini.

Ingawa hizi ada za ziada si sehemu ya kiasi cha pesa taslimu unazolipa mkpeshaji, ni lazima zilipwe na zinafaa kufikiriwa wakati wa kuchagua mkopeshaji. Gharama hizo zinajulikana kama gharama zisizo wazi.

**Ufafanuzi wa istilahi**

Gharama wazi:

Pesa unazomlipa mkopeshaji kwa mkopo uliopata. Ni pamoja na ada, ribaa, bima na ada za kuchelewa kulipa. Kawaida gharama hizi zinakuwa ndani ya kiasi unacholipa kila wiki au mwezi.

Gharami zisizo wazi:

Gharama unazoweza kulipa kwa sababu ya kuwa na mkopo, kama nauri ya kwenda mikutanoni au kwenda benkini. Zinaweza kuwa malipo kwa mfanyakazi wa kusimamia biashara yako wakati umekweda mkutanoni, au kipato unachokosa wakati umefunga biashara kwenda mkutanoni.

Uliza wanafunzi wawili kujitolea kusema gharama walizotambua kwa mikopo yao.

**Uliza:**
Miongoni wa gharama hizo, ni zipi zilizokushtua? Je, kulikuwa na gharama ambazo hukufikiria wakati ukipata mkopo?

Unawezaje kupunguza gharama za mikopo? (panga mapema; fikiria gharama zote za kupata mkopo kabla ya kuchagua mkopeshaji; linganisha wakopeshaji na kuchagua yupi utaweza gharama zake).

## Kipindi 2
Maswali ya kuuliza wakopeshaji

**Uliza:**
Kuna mifano gani ya wakopeshaji mbalimbali katika eneo lako?

Wape nafasi baadhi ya wanafunzi kujibu kabla hujatoa jibu lifuatalo:

- Watu binafsi
- SACCO
- Mashirika ya hifadhi na mikopo
- Kampuni
- Benki ndogo
- Benki kubwa
- Wanunuaji-mazao wanaofanya mkataba na wakulima

Kilimo cha kimkataba ni nini?

Ni makubaliano kati ya mkulima na mnunuaji. Mkulima na mnunuaji hukubaliana mapema juu ya kiasi cha mazao yatakayolimwa na kwa bei gani.

**Ni maswali gani ambayo yanafaa kuulizwa wakopeshaji kabla ya kuamua nani utakopa kutoka kwake?**

Wape nafasi baadhi ya wanafunzi kujibu kabla hujatoa jibu lifuatalo:

- Kiasi cha ribaa ni nini?
- Malipo ya mkopo na ribaa vitalipwa kila baada ya muda gani?
- Kiasi cha kulipa kila mara kitakuwa shilingi ngapi?
- Kiasi gani cha hifadhi kinatakiwa na malipo yatafanyika kila baada ya siku ngapi?
- Ni ada zipi zinazotakiwa kulipwa ili kupata mkopo?
- Ada za kuchelewa kulipa ni shilingi ngapi?
- Malipo ya mkopo yatakuwa yakilipwa wapi? Ni umbali wa kilomita ngapi kutoka kwangu?
- Mikutano inaitishwa kila baada ya siku ngapi? Mikutano hiyo inachukua muda gani?

Dhamana ni nini?

Wape nafasi wanafunzi kutoa majibu yao kabla hujasema jibu lifuatalo:


Dhamana ni mali yenye thamani ambayo inatenda kama bima ya kuthibitisha kwamba utalipa mkopo, la sivyo, mali hiyo itachukuliwa na mkopeshaji. Inaweza kuwa kitu chenye thamani unachotoa mwanzoni na utarudishiwa kitu hicho baada ya kumaliza kulipa mkopo na ribaa, na ukishindwa, mkopeshaji atakuja na kukichota. Kwa mfano, nyumba, ardhi, gari au ng'ombe vinaweza kutumika kama usalama wa mkopo kuhakikisha kwamba unalipa mkopo.

Mdhamini ni nani?

Mdhamini ni mtu wa tatu anayeahidi kulipa mkopo endapo mkopaji atashindwa kuulipa. Mtu huyu lazima awe na rasilimali au pesa zake ili kuthibitisjha kwamba ana uwezo wa kulipa mkopo huo endapo mkopaji atashindwa.

## Kulinganisha wakopeshaji

**Uliza:**
Ni mambo gani muhimu ya kuzingatia unachagua mkopeshaji? Ni kiasi cha ribaa? Aina ya mkopo unaopewa? Mahali mkopeshaji alipo?



Kitabu cha mazoezi: urakasa 20
**Mambo muhimu ya kuzingatia wakati ukichagua mkopeshaji**

Andika mambo matano muhimu (jedwali lililo kwenye kitabu ni mfano; unaweza kuwa na vichwa tofauti chini upande wa kushoto kulingana na yale wanafunzi waliyotaja).

Kisha, panga sifa za kila mkopeshaji kwa utaratibu. Kwa kila sifa, zipange kwa kuzipa alama 1-5 kwenye kisanduku kinachofuata. Fanya hivi kwa sifa zote za kila mkopeshaji kisha jadili utaratibu huo na darasa zima.

**Uliza:**
- Ni sifa zipi ambazo zilipata alama za juu zaidi? Kwa nini sifa hizo ndizo zinapendelewa?
- Weka pamoja sifa zote zilizopata alama za juu zaidi. Mkopeshaji mwafaka anakuwa na sifa gani kwako?

**Uzuri na ubaya wa aina mbalimbali za mikopo**

**Uliza:**
Kupata mkopo kutoka kwa mtu binafsi kuna uzuri na ubaya gani?

Uzuri:
- Utapata mkopo kwaharaka sana kutoka kwa mkopeshaji
- Hatua za kupata mkopo huu ni fupi sana

Ubaya:
- Kiasi cha ribaa ni kikubwa
- Kuna hatari kubwa ya mikinzano (endapo hakuna mkataba ulioandikwa)
- Kuna hatari kubwa kama kupoteza dhamana au adhabu usipolipa mkopo katika muda uliokubaliwa
- Kuharatisha maisha yako na ya familia yako ukishindwa kulipa mkopo

**Uliza:**
Mkopo kutoka shirika la hifadhi na mikopo una uzuri na ubaya gani?

Uzuri:
- Hatua za kupata mkopo ni fupi
- Mkopo hauhitaji dhamana
- Unaweza kupata mikopo midogo

Ubaya:
- Ribaa ya juu kuliko ya benki
- Kupoteza heshima na marafiki katika eneo lako unaposhindwa kulipa mkopo

**Uliza:**
Mkopo wa kilimo cha kimkataba una uzuri na ubaya gani?
Uzuri:
- Kkuna uwezekano wa kupata bima ya mimea
- Kulipwa bei isiyobadirika (hata bei ya mazao ikipunguka katika eneo hilo)
- Ufikikaji wa mkopo

Ubaya:
- Bei iliyokubaliwa mwanzoni inaweza kuwa ndogo ikilinganishwa na ya wakati wa kuvuna
- Hatari kwa wote wawili endapo mavuno ni madogo
- Hatari ya kupoteza dhamana au kupata adhabu endapo umeshindwa kulipa mkopo

**Uliza:**
Mkopo kutoka SACCO una uzuri na ubaya gani?

Uzuri:
- SACCO ni mahali salama pa kupata mkopo
- Unapata mkopo mkubwa kuliko wa shirika la hifadhi na mikopo
- Mkulima binafsi anaweza kupata mkopo

Ubaya:
- Mkopo huu lazima uidhinishwe, kwa hiyo unaweza kukataliwa
- Ribaa na ada za kupata mkopo ni za juu
- Kuna uwezekano wa kupunguzwa kwa kiasi cha mkopo unaotaka


**Uliza:**
Mkopo kutoka benki una uzuri na ubaya gani?

Uzuri:
- Mikataba rasmi inaandikwa, kwa hiyo, hakuna mikinzano
- Unaweza kupata mkopo mkubwa
- Unapewa muda mrefu wa kulipa mkopo (ukilinganisha na muda wa shirika)
- Unapata kiasi kikubwa cha mkopo kuliko cha Shirika na SACCO

Ubaya:

- Hatua za kupata mkopo ni ndefu na ngumu sana
- Ribaa na ada za mkopo ni kubwa
- Hatari kubwa kama kupoteza dhamana au kupewa adhabu kali ukishindwa kulipa mkopo
- Huenda utalazimika kusafiri safari ndefu ili kufika mahali benki ilipo
- Huenda benki haitoi mikopo kwa watu binafsi ila kwa vikundi tu au benkiinaweza kupendelea kukopesha makampuni/biashara badala ya wakulima

**Sifa za mkopaji bora**



Kazi ya vikundi:
**Jiunge na kikundi kisha andika sifa za mkopaji bora**

Wanafunzi wape dakika 5 kufanya kazi hii. Uliza vikundi kuwasilisha majibu yao. Jadili mapendekezo yao kwa kuzingatia majibu yafuatayo:

- Kabla ya kujua ikiwa unaweza kupata mkopo, tayarisha bajeti. Yaani, andika pesa unazotarajia na matumizi kwa wiki au miezi kadhaa ya mbele. Kadiria kiasi ambacho unafikiri unaweza kulipa kila mwezi, wakati pia ukiweza kugharimia mahitaji ya msingi kama chakula, matibabu, gharama za kuendesha biashara na matukio ya dharura
- Mkopo ni deni. Lipa mkopo haraka iwezekanavyo
- Mkopo haupatikani kwa bure. Unatozwa ada mbalimbali. Hesabu kiasi cha pesa ambazo unatakiwa kulipa kwa mkopeshaji pamoja na ada zote na ribaa
- Panga mapema jinsi utakavyolipa mkopo
- Weka kumbukumbu za kila malipo ya mkopo unayofanya
- Usishindwe kulipa kwa muda. Usipolipa humanisha kwamba hutaweza kulipa mkopo kwa muda uliokubaliwa
- Hali hii huwa na athari mbaya, kwa mfano kupoteza ardhi yako, nyumba au mashine za kilimo
- Tafuta habari na ushauri kuhusu mikopo kutoka kwa wanachama wa benki au wa shirika lako
- Usichanganye mikopo ya kibiashara na mikopo unayopata kwa matumizi ya kibinafsi. Ukipata mkopo kwa ajili ya biashara, tumia mkopo huo kwa lengo hilo tu
- Mkopo hutolewa na mkataba. Soma mkataba huo kwa makini kabla ya kutia sahihi. Hakikisha kwamba unafahamu mkataba huo, pamoja na matakwa ya mkopo huo na masharti ya kulipa mkopo huo
- Jiepushe na kupata mkopo kutoka kwa rafiki yako au jamaa yako. Mkopo huo unaweza kuhatarisha uhusiano wenu
- Usipate mkopo kutoka mtu usijemjua. Anaweza kuwa mkopeshaji katili anayetoza ribaa ya juu sana
- Hakikisha una dhamana mwafaka kutoka nje ya biashara yako ya kilimo. Linda biashara yako: ndicho chanzo cha kipato chako
- Pata risiti kila unapofanya malipo kwa mkopeshaji wako ili kujiepusha na fujo na mikinzano




Kazi ya nyumbani:
**Kila mwanafunzi aandike matukio 2 kitabuni akisimulia wakati alipopata mkopo (au alipokopa pesa)**

Usimulizi uzingatie nani alikuwa mkopeshaji, masharti ya mkopo huo, (kiasi cha pesa zilizokopwa, ada za mkopo, kiasi cha ribaa, muda wa kulipia mkopo), lengo la mkopo huo na matumizi ya mkopo; kama aliweza kulipa mkopo huo, kama alipata matatizo)?

Kama kuna mwanafunzi ambaye hajawahi kukopa pesa, anaweza kujaribu kukutana na mtu kutoka eneo lake ambaye amewahi kupata mkopo ili ampe taarifa hizo.

## Kipindi 3

Anzisha kipindi kwa kuuliza wanafunzi kukuonyesha zoezi walilotakiwa kufanyia nyumbani, kagua kama wameandika taarifa za mkopo vyema. Kisha, uliza wanafunzi 3-4 kujadili visa vyao vya mkopo.



Chati 15
**Mchakato wa**

1. Shughuli za kuomba mkopo:

Mchakato huu una madhumuni kadhaa ambayo ni pamoja na:

- Kupata taarifa za msingi kukuhusu ambazo mkopeshaji atazitegemea kuamua kama atakupa mkopo au la.
- Kukusaidia katika kuchagua aina mwafaka ya mkopo

2. Shughuli za kutathmini mkopaji
Mkopeshaji hapa anataka kuthibitisha mambo mawili: kiasi cha pesa unazotaka kukopa na hali yako ya kifedha (mkiwemo mikopo ya nyuma uliyowahi kupata). Mchakato huu unakusanya habari zitakazotegemewa kuamua uwezo wako wa kulipa mkopo na kama kweli una nia ya kulipa mkopo huo. Matokeo ya shughuli hii huandikwa na mkopeshaji ili kufahamu uwezo na nia yako ya kulipa pesa hizo.

3. Shughuli za kuidhinisha mkopo
Mchakato wa kuidhinisha mkopo unabainisha ikiwa mkopeshaji yuko tayari kuhatarisha pesa zake kwa kukupa mkopo, na kwa hiyo kukubali kukupa mkopo. Uamuzi huu unategemea habari zilizokusanywa katika shughuli ya kutathmini mkopaji.

4. Kupokea mkopo
Mkopo ukiidhinishwa, unapokea mkopo, yaani unapokea kiasi cha pesa zilizoidhinishwa.

5. Kufuatilia mkopo
Ukisha pokea pesa za mkopo, ni muhimu sana kwako kuwa unafuatilia kiasi cha pesa unazotakiwa kulipa na lini utahakikisha kwamba umelipa mkopo kulingana na ratiba ya malipo. Mkopeshaji pia atazaidi kuwasiliana nawe na kufuatilia namna ulivyotumia pesa za mkopo.

6. Kulipa mkopo
Katika hatua hii, unatarajiwa kulipa mkopo kama ratiba inavyobainisha kwenye mkataba uliotia sahihi. Ukishindwa kulipa unaweza kukumbwa na matukio yasiyotamanisha. Kwa hiyo, unatakiwa kukopa tu kile kiasi utakachoweza kulipa.



Chati 16a & 16b
**Mkopo wa Rose**

Picha ya 01
Rose nu mwuza-duka. Anauza nguo na mazao kutoka shamba la mume wake. Ana wateja wengi lakini duka lake ni dogo. Anataka kupanua duka lake ili kuweza kujaza bidhaa zaidi humo ili kupata faida zaidi.

Picha ya 02
Rose amekua akiwekeza pesa kwenye kisanduku kwa muda. Ameamua kufungua kisanduku ili kuotoa pesa za kupanua biashara yake. Lakini, pesa alizohifadhi hazitoshi kugharimia bajeti ya makadirio yake.

Picha ya 03
Ameamua kukamilisha kiasi kinachohitajika kwa kupata mkopo kutoka benki/ SACCO ambako ana akaunti.

Picha ya 04
Amepata habari kuhusu mikopo na mahitaji yake. Ana kila kitu kinachohitajika kupata mkopo. Ameanza shughuli za mkopo kwa kuonyesha kitambulisho chake, dhamana, mdhamini, ada za benki, nk.

Picha ya 05
Rose amechukua mkopo wa shilingi za Uganda 500,000/= kutoka benki. Atalipa ribaa ya asilimia 10%. Anataka kulipa mkopo huo na ribaa ndani ya miezi 5.

Picha ya 06
Rose amekagua bajeti yake na kufanya mpango mpya kwa kutegemea pesa alizopokea. Amepangisha chumba kinachojirini duka lake na kujaza bidhaa zaidi.

Picha ya 07
Kuanzia mwezi huu ataanza kulipa, mkopo ule. Anatakiwa kulipa mkopo ndani ya miezi 5. Pesa za mkopo anazolipa kila mwezi ni 100,000. Ribaa ya kila mwezi ni 50,000. Kila mwezi atalipa 150,000 za UGX kwa miezi 5.

Rose anafuata mpango wake wa kulipa mkopo kwa makini na anahakikisha kwamba kila mwezi anapata pesa za kulipa sehemu ya mkopo na ribaa, jumla ikiwa 150,000 za UGX.

Picha ya 08
Hebu tujadili jinsi Rose alivyopanga na kutawala mkopo wake kutoka mwanzoni. Alitayarisha ada za mwanzo za benki (UGX 34,400). Pia aligawa mkopo wake katika miezi 5 ili kuweza kuulipa pole pole. Baada ya miezi 5 alikuwa amelipa mkopo kamili na sasa ana uwezo wa kupata faida zaidi kutoka duka lake ili kuhifadhi au kuwekeza.

**Kushindwa kulipa mkopo**

**Uliza:**
Kushindwa kulipa mkopo ni nini?
Kutolipa kiasi cha mkopo pamoja na ada zingine mkiwemo ribaa ndani ya kipindi kilichokubaliwa huwa umeshindwa kulipa mkopo. Mkopaji aliyeshindwa ni yule anayechelewa kulipa mkopo wake.

**Uliza:**
Kwa nini kushindwa mkoponi shida kubwa? Kwa nini ni muhali kuchelewa siku chache kulipa mkopo?
Wape nafasi wanafunzi wachache kutoa maoni kabla hujatoa majibu yafuatayo:

Kuchelewa siku chache huonekana kama kitu kidogo, lakini siku chache zikigeuka wiki kadha inakuwa vigumu kulipa. Unavyodzidi kuchelewa ndivyo kiasi cha kulipa kinavyozidi kuongezeka, na inazidi kuwa vigumu kupata pesa za kulipa. Unapolipa kwa muda kila wiki au mwezi, huwa unajua muda umewadia na unajitayarisha.

**Sema:**
Mtu mwenye mkopo huwa amevunja mkataba akichelewa kulipa kwa siku moja na zaidi; na pia huwa amevunja mkataba akichelewa kwa miezi 2.

**Uliza:**
Kipi ni hatari zaidi? Siku moja au miezi 2?

(Mkopaji aliyechelewa kulipa kwa miezi 2 hukumbwa na matatizo. Huwa ni dhahiri kwamba ameshindwa kulipa na kiasi anachodaiwa huwa kinaongezeka. Isitoshe, huwa anatakiwa kulipa ada za adhabu ya kuchelewa kulipa).

Shughuli:
**Zifuatazo ni kauli nne zinazotaja matukio fulani, zisomee wanafunzi kisha wape machaguo matatu yaliyopewa.**

Wambie kufikiri na kusema kwa sauti lipi kati ya matunio hayo matatu ni sahihi.

Kabla ya kwenda kwa tukio linayofuata, jadili lile la kwanza na darasa zima.

**Kauli ya tukio la 1:**
Lucky alikopa miliyoni moja na nusu kununua friji ndogo iliyokwisha tumiwa kwa gharama ya UGX 900,000. Mpango wake ulikuwa wa kutumia UGX 600,000 zilizobaki kununua mahindi kwa wingi ili kuyauza na kupata pesa za kutosha kulipia malipo matatu ya mwanzo.

Lakini dada yake Rita alimshawishi amkopeshe zile UGX 600,000 ambazo angemlipa kikamilifu kabla ya muda wa Lucky kufanya malipo ya kwanza ya mkopo. Rita alikimbia na pesa hizo. Lucky alifaa kufanya nini tofauti na vile alivyofanya?

Chaguo la 1:
Kumkopesha dadake pesa baada ya dadake kutoa dhamana yenye thamani iliyozidi pesa zile

Chaguo la 2:
Kukataa kumkopesha dadake na kustahimili hasira za dadake

Chaguo la 3:
Kumkopesha dadake nusu ya hizo UGX 600,000 na kuwekeza zile UGX 300,000 zilizobaki ili kuweza kupata pesa za kulipa mkopo

**Tukio la 2:**
Anya amekopa UGX 350,000 ili kuwekeza kwenye biashara yake ya mboga. Mauzo ni mazuri na amefurahi kwa kuwa anapata faida. Anasherehekea kwa kujinunulia gauni mpya na mpira mpya kwa mtoto wake. Mwishoni mwa mwezi lazima afanye malipo ya mkopo, lakini ana nusu ya pesa zinazotakiwa. Angalifanya kitu gani tofauti na vile alivyofanya?

Chaguo la 1:
Kuweka kando pesa za kulipa mkopo kabla ya kununua zawadi

Chaguo la 2:
Kununua vitu alivyonunua kisha ange-panga kukopa pesa kutoka kwa dadake kujalizia kiasi cha kulipa mkopo

Chaguo la 3:
Angalipata mkopo mkubwa mwanzoni

**Kauli ya tukio la 3:**
John alipata mkopo kutoka benki ndogo katika eneo lake kupanua duka lake. Biashara yake ni ndogo lakini mauzo ni mazuri na amekuwa akilipa mkopo vizuri. Lakini mtoto wake alipopata ajali, alipata mkopo wa dharura kutoka benki ndogo kugharimia matibabu ya mtoto. Kisha alifunga duka lake ili kuuguza mtoto wake nyumbani na hatimaye alishindwa kulipa ile mikopo miwili. John angalifanya nini tofauti na vile alivyofa-nya?

Chaguo la 1:
Angalipata mtu mwingine wa kuuguza mtoto wake ili aweze kuhudhuria duka lake

Chaguo la 2:
Angaliuza kitu kingine cha thamani (k.m. ng'ombe) ili kugharimia matibabu ya mtoto badala ya kupata mkopo mwingine

Chaguo la 3:
Kupandisha bei ya vitu dukani mara mbi-li ili kuweza kupata pesa za kugharimia matibabu ya mtoto

**Kauli ya tukio la 4:**
Michelle aliugua na kulazimika kukaa nyumbani kwa wiki kadhaa. Kwa kuwa hawezi kufanya kazi wakati huu, anapata pesa ndogo zisizoweza kugharimia ma-lipo ya mkopo. Akipata nafuu na kuanza kazi tena, benki itakuwa inamdai pesa zaidi kwa sababu ya ada za adhabu ya kuchelewa kulipa. Kwa sababu ya bidhaa ndogo, Michelle anapata pesa ndogo. Hali inazidi kuwa mbaya na ana hofu hu-enda akalazimika kufunga duka. Michelle angalifanya nini?

Chaguo la 1:
Angeweza kuomba familia yake kuchan-ga pesa za kulipa mkopo wakati akiwa mgonjwa ili asije kulipa ada za kuchele-wa kulipa mkopo

Chaguo la 2:
Kuhifadhi kiasi fulani kila wiki au kila siku mbali na malipo ya mkopo aliyoku-wa akifanya ili kujiepusha na hali kama hii

Chaguo la 3:

Kuwaomba baadhi ya wateja wake kum-saidia kumlipia kiasi cha mkopo kilicho-takikana

**Kufuatilia malipo yako ya mkopo**



Mfano wa 11
**Kisa cha Sara**

Nakili ratiba na malipo ya mkopo katika karatasi kubwa na kuionyesha wanafun-zi, na uliza mmoja wao kuitumia kufanya zoezi hili. Toa maelezo kamili na kuhaki-kisha darasa zima limeelewa.



Kitabu cha mazoezi:
urakasa 21
**Kifaa cha kufuatilia mkopo**




Kazi ya nyumbani:
**Wanafunzi wanakili kielelezo cha kufuatilia malipo ya mkopo kwenye vitabu vyao na kukijaza ikiwa wana mikopo.**



Kuigiza:
**Lengo muhimu ni kuonyesha madhara ya kushindwa kulipa mikopo katika muda uliokubaliwa na kupendekeza njia za kutatua tatizo hili na mkopeshaji**

Wahusika:
- John ni mkulima ambaye ana mkopo kutoka kikundi
- Sam ni mkulima mwingine anayetaka kupata mkopo kutoka kwa kikundi kile mwenyekiti wa kikundi cha kukopehsa
- Wana-chama wa kikundi (kama 2)

Mahali: mkutano wa shirika la kutoa mikopo

Matukio:
- John alipata mkopo kutoka kikundi miezi kadhaa iliyopita. Aliwekeza kwenye biashara ya kuku. Kwa bahati mbaya, kuku wote walikufa. Ameshindwa kulipa mkopo katika muda uliokubaliwa.
- Sam amekuwa mwana-chama wa kikundi kwa muda mrefu. Ameomba mkopo. Angependa kununua mbegu na vitu vingine vya kilimo kwani msimu wa kupanda umeanza
- Mwenye-kiti wa kikundi amemwambia Sam kwamba hawezi kupata mkopo kwa sababu John hajalipa mkopo wake, na kwa hiyo kikundi hakina pesa za kumkopesha
- Sam anakasirika sana. Anamkaripia John na kutishia kunyakua mali yake na kuiuza ili kupata pesa anazohitaji kufanya kazi zake. John naye anajitetea. Anahisi hajatendewa haki kwani anatarajiwaje kulipa mkopo wakati kuku wake wote walikufa
- Mkinzano huu umepamba moto. Wanachama wa kikundi wanaingilia.

Maswali ya kuongoza mjadala:
- Umewahi kusikia tukio kama hili likitokea kwenye kikundi chochote katika eneo lako?
- Kikundi kitakuaje watu wanapokopa pesa na kushindwa kulipa mikopo yao?
- Unafikiri kikundi kimfanyie nini John kwa sababu yameshindwa kulipa mkopo?



Kichemsha ubongo:
**Kweli au si kweli?**

- Pesa za mkopo ni pesa za mtu aliyekopa pesa hizo (si kweli)
- Mkopo unaweza kukusaidia kuanzisha au kupanua biashara ukiwa huna pesa za kutosha (kweli)
- Kama eneo lako limevamiwa na mafuriko, wadudu wanaoharibu mimea au maradhi, kamwe usilipe mkopo wako (si kweli)
- Ukilazimika kufunga biashara yako, si lazima ulipe mkopo wako (si kweli)
- Mwizi akiiba pesa zako zote au kuiba mazao yako, hulazimiki kulipa mkopo wako (si kweli)
- Kutumia pesa zako kuanzisha biashara si ghali sana kama kukopa pesa (kweli)
- Hakuna ada za adhabu za kushindwa kulipa mkopo katika muda uliokubaliwa (si kweli)
- Kiasi cha pesa mtu anazofaa kukopa kinafaa kutegemea kipato chake (kweli)

Kitabu cha mazoezi:
urakasa 23
**Kufasili upya lengo lako**

Wakati ukifunga kikao cha mwisho cha kozi hii, pitia tena malengo ambayo kila mshiriki aliweka mwanzoni mwa mafunzo ambayo wanatarajiwa kuwa wamekuwa wakirekebisha katika kipindi cha wiki 5. Wakiwa na maarifa waliyopata kutoka katika mafunzo haya, washiriki sasa wanapaswa kufasili upya malengo yao ya kuweka akiba kwa kipindi cha wiki 4 cha ukaguzi na tathmini (M&E). Pitia mwongozo kwenye kitabu cha kazi, na hakikisha malengo yao yanawezekana na yamepangwa vizuri kwa njia ambayo kuna uwezekano wa kufanikiwa kufikia malengo yao katika wiki 4 zijazo.

**Muhtasari wa somo**

Deni/mkopo ni nini?
Mkopo ni pesa ambazo mkopaji anaweza kutumia kwa muda fulani. Baada ya kipindi kilichokubaliwa, pesa hizo zinarudishwa kwa mkopeshaji, na mkopaji anaweka ribaa au ada inayotozwa kwa kutumia pesa hizo.

Kwa nini watu wanakopa pesa:
- Kuwekeza
- Kugharimia dharura fulani
- Matumizi ya kibinafsi, kununua kitu fulani ambacho huna pesa zako za kutosha kukinunua

Uzuri wa kupata mkopo:
- Unapata pesa zaidi ya zile ulizohifadhi
- Unaweza kupata pesa kwa haraka sana kama unataka kugharimia dharura
- Mkopo utakuwezesha kuchukua nafasi za kibiashara au kutatua tatizo lililotokea

Ubaya wa kupata mkopo:
- Gharama ya mkopo pamoja na ada zake na ribaa
- Kulazimika kulipa mkopo huo kwa muda uliokubaliwa
- Masharti ya kupata mkopo, k.m. kuwa na dhamana

Kanuni mbili za msingi za kukusaidia kudhibiti deni:
- Usikope pesa usizoweza kulipa.
- Hifadhi pesa kila wakati ili kugharimia dharura ili usilazimike kupata mkopo

**Mwisho wa somo la 07**



Designed by:

PHB

scaling for impact

WFP World Food Programme


UN CDF
Unlocking Public and Private Finance for the Poor

# Mafunzo ya Kifedha


Kozi fupi ya wiki 5

## Kiswahili


# 01 Kitengo 01: maarifa na stadi za kifedha yanahusisha nini?



# 02 Kitengo 02: kuweka malengo




# 03 Kitengo 02: kuwekeza wapi?




# 04 Kitengo 03: kutengeneza bajeti ya familia




# 05 Kitengo 03: mchakato wa kutengeneza bajeti



# 06 Kitengo 03: mapato vs gharama




# Kitengo 04: mobile money ni nini?




# Kitengo 04: jinsi ya kujiandikisha kwa mobile money?



# Kitengo 04: kujua haki zako





Taarifa angavu



Matibabu kwa heshima



Faragha kwa habari ya mteja




Ulinzi dhidi ya watoa huduma wenye hima

# Kitengo 04: kujua wajibu wako




Heshima




Toa taarifa ya sasa kukuhusu wewe mwenyewe



Usitoe rushwa



Kuwa mvumilivu




Ripoti dhuluma yoyote


# Kitengo 04: malalamiko na mifumo ya kutoa majibu







# Kitengo 06: chaguo mbalimbali za uwekezaji








# 13 Kitengo 06: maswali ya kuuliza




MILK
MILK
ILK

# Kitengo 07: mzunguko wa mkopo



# 16a Kitengo 07: mikopo ya Rose

01



02



03





04



05





06

# 16b Kitengo 07: mikopo ya Rose

07



08



WFP World Food Programme

UNCDF
Unlocking Public and Private Finance for the Poor



# Kitabu cha kazi

## Programu ya mafunzo ya uandishi wa habari za kifedha

## Kiswahili

## Ujuzi wa kifedha

Kitengo 01 muhtasari

Ujuzi wa kifedha huwafundisha watu dhana za pesa na jinsi ya kuidhibiti pesa kwa busara. Inampa mtu maarifa, ujuzi na mitazamo inayohitajika ili kupata mazoea mazuri ya kudhibiti pesa yanayohusiana na kupata, matumizi, bajeti, kuweka akiba na kukopa.

Ni muhimu kuwa na ujuzi wa kifedha ili:

- Kufanya maamuzi mazuri kuhusu masuala ya pesa
- Kujua jinsi ya kuweka akiba na kuwa tayari kukabiliana na dharura na matukio yasiyotarajiwa
- Kuweza kukopa pesa (kuchukua mkopo) ili kufanya uwekezaji
- Kupunguza uwezekano wa kufanya maamuzi mabaya ya kifedha ambayo yanaweza kudhuru familia yako na biashara
- Kuwa na maarifa ambayo yanaboresha uelewa wa mtu wa masuala ya kifedha ya kibinafsi
- Kuwa na stadi ambazo zinamwezesha mtu kutumia ujuzi wa kifedha kusimamia fedha za kibinafsi
- Kukuza kujiamini na mtazamo ambao unamwezesha mtu kuwa na uhakika wa kutosha kufanya maamuzi yanayohusiana na fedha za kibinafsi

Kumbuka:
Ujuzi wa kifedha unakuwa muhimu sana wakati tunapotumia maarifa na ujuzi uliopatikana katika maisha yetu ya kila siku, na kuutumia kufanya maamuzi ya busara.

Hii inahitaji mabadiliko kutoka tabia yetu ya sasa:

- Kuishi siku hadi siku
- Akiba bila kusudi
- Kukopa kwa ajili ya dharura
- Kukosa kuchagua kitega uchumi sahihi kwa tabia inayotakikana (k.m. kupanga mpango wa matumizi ya pesa)

Kuwa na ujuzi wa kifedha kunamaanisha kuwa utaweza:

- Kutumia bajeti kudhibiti pesa zako
- Kuwa na mpango wa kuweka akiba na malengo wazi
- Kudumisha akiba kwa ajili ya dharura
- Kuwa na uwezo wa kuchagua njia sahihi ya uwekezaji



## Ndoto zangu





Mfano: ndoto ya Rose
Rose ni muuzaduka anayeuza nguo na bidhaa kutoka kwenyw shamba la mumewe. Ana wateja wengi lakini hana nafasi ya kutosha katika duka lake. Ana ndoto ya kupanua duka lake ili aweze kuuza bidhaa zaidi na kupata faida zaidi.

**Jiulize: una ndoto gani?**

Malengo ya muda mfupi ni yale ambayo yatafikiwa chini ya mwaka 1, kama vile kulipa ada za shule.

**Lengo lako la muda mfupi ni nini?**



Malengo ya muda mrefu  ni yale ambayo yatachukua zaidi ya mwaka 1 kufikia, kama maboresho ya nyumba au kununua nyumba.


**Lengo lako la muda mrefu ni nini?**





Fanya mazoezi!
**Chora na ueleze malengo yako kwenye daftari lako**

## Malengo & akiba

| Lengo la akiba | Kiasi | Lini? | Kila mwezi |
|---|---|---|---|
| *Yaani karo* | *+ 88,000 UGX* | *Kila miezi 4* | *+ 22,000 UGX* |
| | + *UGX* | | + *UGX* |
| | + *UGX* | | + *UGX* |
| *Jumla ya kiasi* | = *UGX* | *Jumla kila* | = *UGX* |



Fanya mazoezi!
**Nakili malengo yako kwenye daftari lako**

Tafadhali kumbuka:

Unapopitia mafunzo, endelea kupitia malengo yako na urekebishe. Mwishoni mwa mafunzo ya wiki 5, fanya marekebisho ya mwisho ukitumia mwongozo katika ukurasa wa 23, na uamue lengo lako litakuwa lipi kwa kipindi cha wiki 4 cha ukaguzi na tathmini (M&E) baada ya mafunzo yako. Lengo lako linapaswa kuwa la kihalisia na linalowezekana kwa kipindi, kwa hivyo hakikisha unaweza kulitimiza!

## Maswali ya kuuliza kwenye benki

**Kufikia akiba yako & uhuru wa kutoa:**

- Ninaweza kutoa pesa mara ngapi?
- Kuna kiasi cha chini kabisa ninacho-takiwa kutoa?
- Akaunti hii ina adhabu gani mtu akitoa pesa?
- Kuna mtandao wa ATM?

**Mahitaji ya kufungua akaunti ya amana:**

- Kiasi gani cha akiba kinachohitajika?
- Ninahitaji hati gani?

**Hali Inayofaa na urahisi wa kutumia:**

- Saa za benki ni zipi?
- Inachukua muda gani kuhudumiwa?
- Wateja wanapata taarifa za akaunti zao? Mara ngapi?
- Mnatoa huduma za simu au za electroniki?

**Usalam:**

- Heshima ya shirika ikoje?
- Kuna bima gani au dhamana ya kulinda pesa za mteja?
- Riba inayopatikana kwenye akiba
- Kuna kiwango gani cha riba kwenye akiba?
- Kinalinganaje na cha mashirika mengine?
- Riba hulipwa mara ngapi?
- Riba inakokotolewaje?

**Gharama ya akiba:**

- Ni ada gani zinazotozwa?

**Kupata:**

- Ni rahisi kiasi gani kutoa pesa kwenye akaunti?
- Kiasi kamili kitapatikana?
- Ada hutozwa ikiwa pesa zimetolewa kabla ya tarehe maalum?



## Akiba

Kitengo 02 muhtasari

**Inabidi tukumbuke kwamba:**

Akiba ni pesa iliyowekwa kando na mtu au kaya kwa matumizi katika siku zijazo.

Kuweka akiba ni ufunguo wa udhibiti mzuri wa pesa, inasaidia mtu na kaya kudhibiti hatari, kukabiliana na dharura, mapato laini, kujenga mali, na kufikia malengo ya kifedha.

Watu huweka akiba kwa kuweka pesa kando wakati inapoingia na kwa kutumia kidogo wakati inatoka.

Unaweza kutumia akiba kukidhi mahitaji yanayotarajiwa na yasiyotarajiwa. Akiba husaidia kulainisha mapato halisi, inaruhusu matumizi ya hiari,pamoja na uwekezaji katika mali na biashara.

Kukiwa na dharura na shida, akiba inakuwezesha kushughulikia hali mara moja.

Akiba inasaidia katika kufikia malengo ya kifedha. Haya yanaweza kujumuisha malengo ya muda mfupi (wiki au miezi) kama vile kununua bidhaa kwa ajili ya biashara, au kulipa ada ya shule, au malengo ya muda mrefu (zaidi ya mwaka mmoja), kama vile kununua ardhi au kujenga nyumba.


**Mazoea mazuri ya kuweka akiba yanayohitajika ni yapi?**


- Tayarisha bajeti ya wiki au mwezi na orodhesha vyanzo vya pesa vinavyotarajiwa na ni pesa ngapi itaingia na pia vitu vitakavyogharimiwa na pesa kwenda
- Panga ni kiasi gani utaweka akiba kila siku, wiki au mwezi na ufuate mpango wako wa kuweka akiba!!
- Kabla ya kutumia pesa yako, jiulize ikiwa unahitaji bidhaa unayotaka kununua. Usiinunue ikiwa huihitaji
- Ikiwa hutumii pesa ambayo unafikiri unapaswa kutumia, weka pesa hiyo kando kwa matumizi ya baadaye. Usiitumie tu kwa sababu unaweza!
- Kuweka akiba pesa kidogo tu ni bora kuliko kutoweka chochote
- Weka kumbukumbu za kiasi ambacho umedunduiza na kiasi ambacho ametumia kila siku, wiki au mwezi
- Angalia mazoea yako ya matumizi ya pesa na uamue jinsi unavyoweza kupunguza ili uweze kuweka akiba zaidi
- Weka akiba yako katika benki, SACCO au chama cha akiba na mkopo. Hii itakusaidia kutofikia pesa zako, na hivyo itakuwa rahisi kuweka akiba



**Kanuni za kawaida kwa uwekaji akiba:**

- Udhibiti wa pesa unategemea sana nidhamu yako ya kibinafsi
- Weka akiba mara tu unapopata  pesa. Yaani, kuweka akiba kando kabla ya matumizi
- Jaribu kuweka 10%-20% ya kipato chako (k.m. kwa kila UGX 100,000 weka kiasi cha chini kabisa UGX 10,000 -20,000)
- Usibebe pesa nyingi; epuka kishawishi cha kuzitumia!
- Tumia kwa uangalifu
- Weka akiba mahali pasipofikika, mahali salama
- Lipa madeni
- Weka kando akiba ya dharura








**Kumbuk:**

- Mazoea mazuri ya uwekaji akiba yanahitaji nidhamu
- Nidhamu inatokana na mazoea!

## Mapato vs. matumizi

|  Tarehe |  Mapato |  Matumizi |
|---|---|---|
| | + | + |
| | + | + |
| | + | + |
| | + | + |
| | + | + |
| | + | + |
| | + | + |
| Jumla ya kila: | = | = |

## Bajeti ya familia

| Mapato | UGX |
|---|---|
| Shirika la misaada | |
| Mapato ya Biashara | |
| Mapato ya shambani/mshahara | |
| Nyingine (kuuzia WFP chakula n.k.) | |
| Jumla | = |

| Matumizi | |
|---|---|
| Akiba | |
| Kulipa madeni | |
| Kulipa mikopo (VSLA / benki) | |
| Wakopeshaji pesa | |
| *Gharama za lazima za kaya* | |
| Chakula | |
| Makaa | |
| Sabuni/sodo usafiri | |
| Karo | |
| Vifaa vya masomo | |
| Zingine (sola, kusaga nafaka, n.k.) | |
| *Matumizi ya kibiashara* | |
| Ugavi | |
| Mengine (kodi, usafirishaji, n.k.) | |
| *Gharama za hiari* | |
| Mavazi | |
| Zingine (vyombo, kusuka nywele, n.k.) | |
| Jumla | = |

## Ufuatiliaji wa pesa kila siku

| Tareh | Pesa za kuanzia | Mapato | Akiba | Matumizi | Pesa za kumalizia |
|---|---|---|---|---|---|
| Jumatat | | + | - | - | = |
| Jumann | | + | - | - | = |
| Jumatano | | + | - | - | = |
| Alhamisi | | + | - | - | = |
| Ijuma | | + | - | - | = |
| Jumamo | | + | - | - | = |
| Jumapil | | + | - | - | = |
| Jumla kila wiki | | = | = | = | = |

## Uwekaji bajeti: udhibiti wa fedha za kibinafsi

Kitengo 03 muhtasari

- Kuelewa mahitaji ya kifedha ya kaya
- Kufuatilia uingiaji wa pesa na matumizi
- Kuweka malengo ya kifedha
- Kuunda mpango wa kifedha na bajeti

**Kumbuka:**
Bajeti ni muhtasari wa mapato yanayokadiriwa na jinsi yatakavyotumiwa kwa muda uliowekwa.

**Manufaa ya upangaji wa kifedha wa kibinafsi:**

- Husaidia mtu kuamua vipaumbele vya matumizi ya pesa katika siku zijazo
- Humpa mtu nidhamu katika kutumia pesa na kuweka akiba
- Hukusaidia kukwepa upungufu wa pesa usiotarajiwa
- Hukusaidia kutohisi wasiwasi wa kifedha

**Vitu vitatu unavyoweza kufanya ukitumia pesa:**

- Unazitumia kwa mahitaji ya kila siku kama vile chakula, nyumba, usafiri, mavazi, huduma ya afya, ulipaji wa madeni, na mahitaji mengine ambayo sio muhimu kama vile kunywa pombe
- Weka akiba ya pesa kwa matumizi yasiyotarajiwa k.m. dharura, bili za matibabu, kifo, mtu anayeuza mali zake kwa sababu ya dharura
- Wekeza pesa kwenye shughuli zinazoingiza kipato ili kupata mapato katika muda mrefu

**Jinsi ya kufuata mpango wako:**

- Jikumbushe kila mara kuhusu kitu ambacho ulipanga kugharimia
- Weka katika mpango wako kitu kidogo kwa ajili ya mahitaji ya matumizi ya pesa yasiyotarajiwa
- Weka akiba yako mahali ambapo hapafikiki upesi ili kuepuka gharama ambazo hazikupangwa
- Fuatilia pesa unazotumia, hakikisha hutumii zaidi ya kiasi ulichopanga kutumia
- Ishirikishe familia yako katika kupanga na kuufuata mpango

**Njia za kupunguza matumizi:**

- Nunua vitu visivyo mahitaji ya msingi (kama vile pombe) kwa uchache
- Punguza gharama na utumie pesa kwa wastani kwa ajili ya hafla za maisha kama vile ndoa, mazishi na aina zingine za matukio
- Panga mapema kununua mahitaji wakati bei zikiwa chini na usinunue vitu vingi kwa deni
- Beba pesa kidogo au weka pesa mahali salama ili uepuke kishawishi cha kuzitumia



## Huduma za kifedha

Kitengo 04 muhtasari

Huduma za kifedha hutolewa na benki, mashirika madogo ya fedha, SACCO, VSLA, wakopeshaji  pesa na wengine.

Akiba:
Aina tofauti za akaunti zinapatikana katika mashirika tofauti ya kifedha (kwa mfano akaunti za kawaida na za amana za kudumu)

Mikopo:
Mashirika tofauti ya kifedha hutoa aina tofauti za mikopo kwa masharti tofauti kwamakusudi tofauti.

Bima:
Huduma za bima hushughulikia matukio maalum, .k.m. ajali au kifo

Huduma za malipo:
Mashirika huhamisha pesa kutoka kwa akaunti ya mteja kwenda kwa mpokeaji aliyeteuliwa, k.m. malipo kwa wanafamilia au malipo ya bili

**Huduma za benki kwa mawakala**
Huduma za benki kwa mawakala ni hali ambapo benki ya kibiashara inatumia wakala kutoa huduma za kifedha kwa niaba ya benki nje ya njia za awali za kutumia wahesabu pesa, mashine za ATM na majengo ya benki. Mifano ya mawakala wa benki ni pamoja na wafanyabiashara, SACCO na wengine

**Kumbuka:**
- Daima kufika ukiwa na kitambulisho chako ili kutoa pesa (k.m. hati ya us hahidi wa ukimbizi)
- Kila mara muulize wakalaikiwa ana pesa za kutosha kabla hujafanya shughuli
- Tumia ama alama ya vidole na/ au pini ili kutoa pesa au kununua chakula
- Omba risiti inayotolewa na mashine, hata kama huduma itashindikana. Kila mara weka risiti za shughuli zako zote
- Omba kusaini au kuandika jina lako kwenye kitabu cha mawakala baada ya kila shughuli Hakikisha unathibitisha kuwa umepokea kiasi sahihi cha pesa kabla ya kusaini katika kitabu cha wakala.
- Umepoteza/shida yoyote na kadi yako ya benki? Ripoti mara moja

**Usifanye:**
- Kamwe usiandike PIN yako mahali ambapo mtu anaweza kuipata. Afadhali uikariri.
- Kamwe usiweke namba  yako ya siri ya PIN pamoja na kadi yako ya benki
- Kamwe usimwambie mtu yeyote namba yako ya siri, hata watoa pesa au mfanyabiashara
- Kadi yako ya benki itazuiwa ukitumi namba ya siri isiyo sahihi mara 3.
- Kamwe usimwachie wakala wa Benki kadi yako au  namba ya Pini
- Kamwe usitumie smart card  yako kama dhamana ya kufikia pesa au bidhaa kwa mkopo
- Kamwe usilipe pesa kwa mawakala kama malipo ya benki, malipo yanaweza kukatwa moja kwa moja kutoka kwenye akaunti yako wakati wa mchakato wa kufanya shughuli

**Mobile money**

- Kamwe usimpatie mtu yeyote PIN yako au kuweka PIN yako pamoja na SIM kadi yako

- Kila mara taka  kuangalia karatasi ya malipo kwa viwango tofauti vya shughuli za kutoa na kutuma pesa

- Kila mara hakikisha kiasi  na jina la mtu ambaye unamtumia pesa, kabla ya kuingiza PIN yako

**Kujua haki zako na wajibu**

Kama wateja wa shirika la kifedha (k.m. SACCO, benki n.k.) lazima uelewe haki zako (unachostahili kama mteja wa shirika la kifedha) na wajibu.

**Haki:**

- Kusikilizwa kukiwa na tatizo
- Kutendewa kwa heshima.
- Kupokea habari kamili, sahihi na inayoeleweka
- Kulindwa dhidi ya watoa huduma za kifedha wenye hima
- Inabidi kuwepo hali ambayo ni  rahisi na inafaa kwako kupata pesa zako
- Habari yako inapaswa kuwekwa kwa faragha

**Wajibu wako:**

- Toa habari sahihi kukuhusu na kuhusu familia yako
- Heshimu na kufuata sheria na kanuni za watoa huduma ya kifedha
- Kuheshimu watoa huduma na wabia wengine
- Uadilifu: Usitoe rushwa au zawadi zozote ambazo hazikuandikwa kama sharti la kupata huduma
- Ripoti dhuluma yoyote
- Kuwa na subira patience

**Ukiwa na malalamiko:**

- Taka kujua namba ya simu isiyo ya kulipiwa ya shirika linalotoa huduma za kibinadamu, shirika bia tekelezi, watoa huduma za kifedha ili utoe  malalamiko yako. Kwa mfano, 0800 210 210 ni namba ya simu  kwa WFP na 0800 323 232 ni namba ya simu kwa UNHCR

- Tumia madawati ya madai ambayo hushughulikia maswala mengi mkiwemo malalamiko


- Shiriki katika mikutano ya jamii na kanda ili kutoa  malalamiko yako miongoni mwa mambo mengine

- Kwa wale wanaojua kuandika, weka malalamiko yako kwenye masanduku ya maoni yaliyowekwa katika sehemu tofauti za usambazaji na katika ofisi za watekelezaji

- Tumia fomu za kawaida za rufaa za ulinzi ambazo viongozi wa Wakimbizi wanakuwa nazo ili kutoa  malalamiko yako

- Tumia kliniki za malalamiko zitembeazo kwenye jamii yako

- Tumia mifumo mingine ya kupata maoni kama mikutano  mingine ya  umma na ya kifedha, redio za umma, uchunguzi wa kimsingi n.k.



## Mfano wa shughuli za uzalishaji kipato


- Kuoka mikate
- Kutengeneza baiskeli
- Upikaji pombe
- Uchinjaji
- Kutunza nyuki
- Uhunzi
- Kutengeneza matofali
- Useremala
- Kuuza matofali ya mavumbi
- Kuuzaji samaki
- Kuchoma samaki
- Kupika chapati
- Kufuga mbuzi
- Kutengeneza mafuta ya njugu
- Kusuka nywele
- Ufumaji
- Uashi Kutengeneza mikeka
- Kuchoma nyama
- Kusaga nafaka
- Ufinyanzi
- Ufugaji kuku
- Kununua na kuuza mazaoa
- Kuuza nguo za mitumba
- Bustani za miche
- Kutengeneza viatu
- Kutengeneza sabuni
- Ushonaji Mkahawa
- Kupanda mboga
- Tanuri mikate

























Fanya mazoezi!
**Chaguo zako 3 za juu ni zipi? Kwa nini?**

## Sababu za kufanikiwa au kushindwa

| **Sababu za kufanikiwa** | **Sababu za kushindwa** |
|---|---|

*Maarifa, stadi na upatikanaji wa muda*

| | |
|---|---|
| Ujuzi mzuri wa biashara | Kutokuwa na ujuzi<br>Kutojua wapi pa kuuza bidhaa<br>Kutokuwa na taarifa<br>Kushindwa kutenganisha fedha za biashara na za kaya |

*Soko na wateja*

| | |
|---|---|
| Utashi wa msimu wa kutabirika<br>Utashi wa juu wa mazao<br>Matangazo mazuri<br>Ushindani<br>Bidhaa bora<br>Uhusiano mzuri na wateja<br>Msingi mzuri wa wateja | Kuuza kwa mkopo<br>Ushindani mkubwa sana<br>Mahali duni<br>Wateja wachache |

*Mapato: shuguli ya kuzalisha mapato inaleta faida?*

| | |
|---|---|
| Uelewa mzuri wa mahitaji ya soko | Kuanza bila lengo au mpango<br>Kodi za juu |

*Chanzo cha mtaji*

| | |
|---|---|
| Upatikanaji wa mtaji wa kuanzia<br>Kufikia huduma za kifedha (rasmi na zisizo rasmi) | Mtaji wa kuanzia usiotosha<br>Kutokuwa na akiba<br>Madeni mengi<br>Ufikiaji mdogo kwa huduma za kifedha |

*Mapato ya kaya*

| | |
|---|---|
| Lipa gharama za kaya na mapato ya kaya bila kutumia sana faida ya biashara<br>Msaada wa kifedha kutoka kwa wanafamilia | Mapato ya chini ya kaya hupelekea utoaji pesa kutoka kwenye biashara |

## Mambo muhimu matano kabla ya kuchagua shughuli ya kuzalishia kipato

**1. Maarifa, stadi & muda**
Nina maarifa na stadi kwa shughuli yangu ya kuzalishia kipato na kuna wafanyakazi wa kuiendesha?



**2. Soko & wateja**
Kutakuwa na watu wa kutosha kununua bidhaa au huduma yangu?




**3. Uwezekano wa kupata**
**Faida kutokana na biashara yangu?**




**4. Chanzo cha mtaji**
Nina pesa za kutosha kuanzisha na ku-endesha shughuli ya kuzalishia kipato?

**5. Mapato ya kaya**
**Mapato kutokana na shughuli ya kuzalishia kipato pamoja na mapato mengine ya familia yatatosha kulipia gharama za kaya?**







## Kupanga biashara

Shughuli za lazima ukitaka kuanza:

*(weka wazo lako la biashara hapa)*

| Mwezi | 01 | 02 | 03 | 04 | 05 | 06 | Nani? Ninit? |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kupanga | | | | | | | |
| Shughuli za kuanzia | | | | | | | |
| Shughuli | | | | | | | |

*Kumbuka:*
*Taja shughuli za lazima kwa kila hatua ambazo ni maalum kwa wazo lako la biashara!*



## Shughuli zinazoongoza mapato: uteuzi, upangaji na usimamizi

Kitengo 05 muhtasari

Shughuli ya uzalishaji kipato ni nini? Hii ni biashara inayoendeshwa na kusimamiwa na mtu binafsi au kikundi cha watu kwa madhumuni ya kupata faida ili kuongeza mapato ya kaya.

**Mambo matano muhimu ya kuzingatia kabla ya kuchagua shughuli ya kuzalishia kipato**

1. Nina maarifa, stadi na muda kwa shughuli hiyo ya kuzalishia kipato?

2. Nitapata watu wa kutosha kukunua bidhaa au huduma zangu?

3. Shughuli ya kuzalishia kipato itazalisha pesa za kutosha kulipia gharama na nipate faida pia?

4. Nina mtaji wa kutosha kuanza na kuendesha shughuli ya kuzalishia kipato?

**5. Kipato kutoka katika shughuli ya kuzalishia kipato pamoja na mapato ya familia yatatosha kulipia gharama za familia?**

**Kwa shughuli ya kuzalishia kipato yoyote iliyochaguliwa, ni muhimu sana kuzingatia yafuatayo:**

Jina la biashara
Chagua jina la biashara ambayo unakusudia kufanya k.m. chapati.

Vyanzo vya fedha
Onyesha ni wapi pesa za kufanyia biashara zitatoka

Bidhaa na huduma:
Ni bidhaa au huduma gani ungependa kutolea soko?

Soko kwa bidhaa/huduma:
Tambua wateja wako wa lengo watakuwa nani


Washindani tambua ni nani aliye katika biashara hiyo hiyo na wewe? Je! Ni udhaifu na nguvu zao gani? Je! Ni faida yako ya ushindani?

Mchanganuo wa sekta
Kuelewa sekta (kilimo au isiyo ya kilimo) ambayo unataka kufanya kazi. Je! Ni faida gani au inaudhi biashara uliyonayo

Uchambuzi wa mahitaji
Je! Mahitaji yamekuwaje katika kipindi kilichopita (kuongezeka au kushuka) ni wateja tu wa ndani au wewe unayo wa nje pia?

Uchambuzi wa ugavi
Pembejeo zako (hisa au mbegu na mbolea) zitatoka wapi?

Usimamizi
Nani atachukua malipo kamili ya usimamizi wa biashara?



## Maswali ya kuuliza kabla ya kufanya uwekezaji


- Uwekezaji unafanyaje kazi? Unaelewa kitega uchumi chako vizuri sana kiasi cha kuweza kumwelezea mtu mwingine?



- Malengo yako ni yapi? Unatafuta usalama, mapato au kukua? Au vyote viwili kukua na mapato?
- Kuna hatari gani za kitega uchumi hiki? Unaridhika na hali ya kubahatisha?



- Unategemea kupata kiasi gani cha mapato kutokana na kitega uchumi hiki? Je, hii inawezekana?
- Unapanga kuwekeza kwa muda gani? Huu ni uwekezaji wa muda mfupi, wa wastani au wa muda mrefu?



- Gharama za kununua, kushikilia na kuuza kitegauchumi ni zipi? Utalipa ushuru ukitumia pesa unazopata?
- Una vitegauchumi gani vingine tayari? Kitegauchumi hiki kinaambatanaje na vitegauchumi vyako vingine? Je, kitabadilishaje mchanganyiko wako wa mali?



## Vitegauchumi

Kitengo 06 muhtasari

Uwekezaji ni nini?

- Uwekezaji ni kitendo cha kuweka rasilimali kwenye shughuli fulani ukiwa na matarajio ya kuziwezesha rasilimali zako kukua.

- Kitegauchumi kinaweza kuwa aina ya mali kama vile mifugo (ng'ombe, mbuzi, nguruwe), nyumba (nyumba za kukodisha), biashara (vibanda vya soko, maduka ya vyakula, boda boda) ambayo unaweza kutumia kujipatia faida

Kwa nini unawekeza?

- Kutengeneza mali
- Kuongeza uwezo wa kuchuma kipato
- Kubuni kazi kwa ajili yako mwenyewe, familia na wengine
- Vyanzo vya pesa kwa vitegauchumi
- Mikopo
- Ruzuku
- Faida zilizowekezwa upya

Kudhibiti hatari

• Kila kitega uchumi kinakuwa na hatari. Kuna hatari ya kupoteza pesa, kuibiwa, kusimamiwa vibaya, kuharibiwa.

• Fuatilia vitega uchumi vyako kwa makini ili kuhakikisha kuwa havikupotezei pesa na muda

• Mseto wa chaguzi za uwekezaji. Usiweke mayai yako yote kwenye kikapu kimoja! Kwa mseto unapunguza hatari kwa kuieneza kwa aina tofauti za uwekezaji.

• Una uwezo wa kupata kipato zaidi wakati hatari ikiwa juu na kinyume chake.

Maswali ya kuuliza kabla ya kufanya uwekezaji:

• Kitega uchumi kinafanyaje? Je, unaelewa kitega uchumi hicho vya kutosha kuweza kumwelezea mtu mwingine?

• Malengo yako ni yapi? Unatafuta usalama, mapato au kukua? Au yote viwili kukua na mapato?

• Kuna hatari za kitegauchumi hiki? Unaridhika na hali ya kubahatisha?

• Unategemea kupata kiasi gani cha mapato kutokana na kitegauchumi hiki. Je, hii inawezekana?

• Unapanga kuwekeza kwa muda gani? Huu ni uwekezaji wa muda mfupi au wa muda mrefu?

• Gharama za kununua, kushikilia na kuuza kitegauchumi hiki ni zipi? Utalipa ushuru ukitumia pesa unazopata?

• Una vitegauchumi gani vingine tayari? Kitegauchumi hiki kinaambatana vipi na vitegauchumi vyako vingine? Je, kitabadilishaje mchanganyiko wako wa mali?




## Mambo muhimu ya kuzingatia wakati ukichagua mkopeshaji

| Mkopeshaji | 01 | 02 | 03 |
|---|---|---|---|
| Kiasi cha riba | | | |
| Nafasi ya kupata mkopo | | | |
| Aina ya mikopo inayotolewa | | | |
| Umbali kutoka nyumbani kwangu nguhome | | | |
| Marudio ya malipo | | | |
| Upatikanaji wa huduma zingine | | | |
| Muda wa | | | |



## Kifaa cha kufuatilia mikopo

| Mkopeshaji |  Mkopo 01 |  Mkopo 02 |  Mkopo 03 |
|---|---|---|---|
| Tarehe mkopo ulipopokelewa | | | |
| Kiasi cha mkopo | | | |
| Riba % | | | |
| Kipindi cha mkopo | | | |
| Fungu la kulipa | | | |
| Kiasi kilicholipwa (mwezi 01) | | | |
| Kiasi kilicholipwa (mwezi 02) | | | |
| Kiasi kilicholipwa (mwezi 03) | | | |

Kumbuka: ongeza miezi ikihitajika

## Mikopo: kushughulikia deni kwa mafanikio

Kitengo 07 muhtasari

Watu hukopa pesa ili kuwekeza, kushughulikia dharura isiyotarajiwa au kununua bidhaa ambayo huna pesa za kutosha za kuinunua. Mkopo ni pesa ambazo mwenye kukopa anaweza kutumia kwa muda, na baada ya muda uliowekwa pesa hizo hurejeshwa kwa mmiliki - kawaida pamoja na riba au ada inayotozwa kwa anayekopa kutumia pesa hizo.

Mkopo utakusaidia kutumia fursa za uwekezaji au kutatua tatizo au shida ya papo hapo kwani inatoa pesa nyingi kuliko ulizonazo kwenye akiba, na inatoa fursa ya kupata pesa haraka wakati unazihitaji kwa dharura.

Mikopo ilikuwa na riba na ada pamoja na wajibu wa kulipa mkopo wako kwa wakati. Kunaweza pia kuwa na takwa la dhamana kabla ya kupata mkopo (mali nk).

**Tabia nzuri za kukopa:**

- Kabla ya kujua ikiwa unaweza kuchukua mkopo, tengeneza bajeti ya kuorodhesha mapato yako yanayotarajiwa na gharama kwa wiki au miezi ijayo. Kadiria ni kiasi gani unafikiri unaweza kulipa kila mwezi, pamoja na kulipia vitu muhimu kama chakula, bili za matibabu, gharama za biashara na dharura
- Mkopo ni deni. Lipa mapema haraka iwezekanavyo na epuka kukosa - kutoweza kulipa mkopo kwa wakati. Hii ina athari mbaya sana, kama vile kupoteza ardhi yako, nyumba au vifaa vya kilimo
- Mkopo sio pesa za bure! Unakuwa na gharama. Hakikisha unajumuisha ada na riba pamoja na kiasi cha pesa ambacho lazima umrudishie mkopeshaji
- Usikope zaidi ya unavyoweza kulipa!
- Panga mapema jinsi utakavyolipa mkopo na uweke kumbukumbu na risiti za ulipaji wako wa mkopo kama ushahidi
- Uliza wakopeshaji wa mikopo, mashirika ya kifedha au memba wa vyama vya ushirika kwa habari kuhusu mikopo. Enda huku na huko na uangalie chaguzi tofauti za mkopo kabla ya kuamua chaguo bora
- Usikope kutoka kwa mtu ambaye hujui na epuka kukopa kutoka kwa rafiki au mtu wa familia. Hii inaweza kuharibu uhusiano wenu
- Usichanganye mikopo ambayo unachukua kwa ajili ya biashara na ile unayochukua kwa sababu za kibinafsi. Ukichukua mkopo kwa madhumuni ya biashara, utumia kwa madhumuni ya biashara tu
- Mkopo unakuwa na mkataba. Usome mkataba kwa makini kabla ya kusaini. Hakikisha unauelewa mkataba, pamoja na matakwa ya mkopo na masharti ya ulipaji
- Weka akiba ya pesa mara kwa mara kwa dharura ili kuepuka kukopa pesa




## Kuweka malengo madogo lakini ambayo yanaweza kutimizwa!

**1. Fafanua lengo lako la kuweka akiba**
Je, unataka kutimiza nini katika wiki 4 zijazo? Tumia ujuzi wako mpya na uwe wa kweli wakati ukiweka lengo lako ili kuhakikisha kuwa unaweza kufuata na kukamilisha lengo lako. Hili ni kazi ya kufanya mazoezi ya tabia ya sio tu kuweka malengo ya muda mfupi, lakini pia kujenga ujasiri wako na kuhakiki-sha kuwa kuweza kutimiza malengo yako. Baada ya muda, unaweza kuweka malengo makubwa zaidi, lakini lazima uwe na mwanzo fulani!





**2. Ninahitaji kiasi gani?**
Sasa unajua jinsi ya kutengeneza bajeti na kupanga, kwa hivyo weka mpango wa akiba wa wiki nne unaowezekana ambao utakuruhusu kufikia lengo lako. Kuwa wa kweli na mwaminifu kwako mwenyewe. Rekebisha lengo lako vizuri ukigundua huna njia inayohitajika kufikia lengo lako.




**3. Ratiba**
Hakikisha unapanga ama kila siku au kila wiki kwa kipindi cha wiki nne. Weka ratiba yenya malengo wazi ya kuweka akiba ambayo yanaambatana na mapato yako yanayotarajiwa.



**4. Madhumuni ya lengo langu ni nini?**
Tafakari juu ya sababu ya kuweka lengo hili mahsusi. Jiruhusu kufikiria muda mrefu zaidi na ufikirie mbele. Baada ya kufanikiwa kutimiza lengo hili, nini kinafuata?




## Kila la heri!



Designed by:

PHB

scaling for impact